MAWAKILI WA SIRI

Wahuduma wa siri

Siri ya utauwa ni kuu

Kubadilishwa kwa watakatifu

Sehemu nne za neema - sehemu mbili za ukweli

Farijianeni kwa maneno hayo

Ufalme wa Mungu, kuja kwa Bwana, ujumbe wa uwana.

Ufunuo wa kitume

Kwa nini uwana?

Kujua neema ya Mungu

Mtazamo wa mafundisho ya uwana

Baraka tano za Baba

Maombezi kubwa

YALIYOMO.

Ukurasa

1. **Utangulizi** 3
2. **Wahuduma wa Siri** 6
3. **Siri ya utauwa ni kuu!** 10
4. **Kubadilishwa kwa watakatifu** 14
5. **Sehemu nne za neema - sehemu mbili za ukweli** 18
6. **Farijianeni kwa maneno haya** 23
7. **Ufalme wa Mungu, kuja kwa Bwana, Ujumbe wa uwana** 28
8. **Ufunuo wa kitume** 32
9. **Kwa nini uwana?** 36
10. **Mtazamo wa mafundisho ya uwana** 38
11. **Kujua neema ya Mungu** 43
12. **Baraka tano za Baba** 46
13. **Maombezi kubwa** 50

UTANGULIZI

Maarifa ya siri

"***Mtu na atuhesabu hivi, kuwa tu watumishi wa Kristo, na mawakili wa siri za Mungu"*** **1 Wakorintho 4:1.** Msemo wa ajabu jinsi gani! Na ni nani atajaribu kukubali fulsa na jukumu hii ya ajabu kuwa **mtumishi wa Masihi na wakili wa siri za Mungu?**

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa ***"Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni"*** **Mathayo 13:11.** Akazidi kusema "***Heri macho yenu, kwa kuwa yanaona; na masikio yenu, kwa kuwa yanasikia. Kwa maana, amin, nawaambia, Manabii wengi na wenye haki walitamani kuyaona mnayoyaona ninyi"*** **aya 16-17.**

Mitume wa kwanza na manabii walipewa ufahamu wa siri, kwanza na Yesu kwa wale kumi na wawili na kisha na Roho Mtakatifu kwa wale waliofuata baadaye (**Efe 3:5**). Kanisa la kwanza lilijengwa juu ya Msingi wa manabii na mitume **Efe 2:20** waliokuwa na maarifa ya siri.

Hata hivyo maarifa haya ya siri yalipotea wakati kanisa kihistoria lilikataa kwanza mitume na kisha manabii. Katika siku hizi za mwisho Mungu anapokamilisha kazi yake ya urejesho, tunawakaribisha tena mitume na manabii kuhudumu miongoni mwetu ili watujuze "***Hekima ya Mungu".*** Hekima hii ni ya waliokomaa (**1Wakorintho 2:6-7**)

Kuwaleta watakatifu katika urithi

Paulo anatuambia kwamba maarifa ya siri "***Ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote"*** **Efe 3:9.** Maarifa haya ya siri ni "***hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu"*** **1Wakorintho 2:7.** Paulo alisema ***"Ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo"*** **Efe 3:3.** Paulo pia anasema kuwa ufunuo huu ulimjilia kwa sababu "***ya uwakili wa neema ya Mungu niliopewa kwa ajili yenu"*** **Aya 2.**

Paulo ako wazi kwamba uwezo wake wa kuhudumu ulikuwa ni kulingana na kipawa cha neema ambayo alikuwa amepokea (**Efe 3:7**). Katika **Wakolosai**, Paulo tena alitaja juu ya uwakili ama neema ambayo alikuwa amepokea ambayo ilimuwezesha "***kulitimiza neno la Mungu; siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake; ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu"*** **Wakolosai 1:25-27.**

Siri kwanza inafunuliwa kwa mitume na manabii, lakini kusudi lake ni ijulishwe **Watakatifu!** Maarifa ya siri ni **urithi wa watakatifu wote** na, pasipo maarifa ya siri, hatuwezi kurithi na kuja katika ukomavu /utimilifu ambao Mungu amekusudia.

Ushirika wa uwana

Wakati watakatifu wamepokea maarifa ya siri, watakatifu kisha wanaweza kushiriki hayo maarifa. Paulo anaiweka kwa njia ingine katika **Waefeso**: "***Kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika; na kuwaangazia watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo"*** **Efe 3:8-9.**

Wakati tunakuja kujua siri tunaingia katika ushirika wa ndani (*Koinonia*). Huu ndio ushirika wa kujua ya kwamba tu **wana**, tukiisha kupokea "***Kufanywa wanawe"*** **Efe 1:5,** tukiisha kupokea "***Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, …si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana basi, u mrithi wa Mungu"*** **Gal 4:6-7.** Yesu anatakiwa kuwa "***Mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi"*** **Rum 8:29** na kupitia yeye "***Mungu anawaleta wana wengi waufikilie utukufu"*** **Ebr 2:10.** Kusudi la Mungu ni **Wandugu** wakue katika ukomavu, wakiwa

tayari kupokea **hekima ya ndani** kama wana, ambao watafunuliwa ulimwenguni wakiuonyesha utukufu wa Mungu (**Kol 1:27, Rum 8:19**).

Mausia ya Mungu

Petro anatueleza sisi wote tuwe ***"mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu"*** **1Petro 4:10,** tukihudumiana mmoja na mwingine kulingana na karama tulizopewa. Wakati watakatifu wamefunzwa vyema na kufundishwa **hekima ya ndani**, kisha kila mtakatifu anafanyika mhuduma na njia ya kuhudumu ni kupitia neema. Karama ambayo Kristo anapeana kwa kila mmoja inahudumiwa katika moja ya njia mbili: ***"Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu"*** **1Petro 4:11.**

Kunena **kama mausia ya Mungu** inaonyesha 'kujulisha siri'. **Mausia** ya Mungu ni neno halisi la Mungu. Mwanzo wa neno hili *mausia*, katika Kiebrania, inazungumza juu ya Mungu akizungumza kutoka mahali patakatifu pa patakatifu (**Kutoka 25:21-22**). Kwa hivyo inazungumzia **hekima ya ndani, siri**.

Kumbuka kulikuwa ni kukiri kwa Petro, ***"Wewe ndiwe Kristo, mwana wa Mungu aliye hai",*** huu ndio msingi wa ufunuo wa msingi wa siri ya 'Yesu ni nani?'. Juu ya ufunuo huu kanisa linajengwa (**Mathayo 16:16-18).**

Kila mwanafunzi akiwa na uwezo wa kuhubiri

Philipo, mmoja wapo wa wale saba (**Mdo 6**), alikua chini ya mitume wa kwanza na alikuwa mmoja wa wanafunzi ***"waliotawanyika"*** wakati mateso yalitokea wakati Stefano aliuawa **(Mdo 8:1-4**). Maandiko yanasema "***walienda kila mahali wakilihubiri neno".*** Philipo alikwenda Samaria "***akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu na jina lake Yesu Kristo"*** **Mdo 8:12.** Ilikuwa na tofauti ipi mahubiri ya Philipo na mahubiri ya kawaida katika karne ya ishilini na ishilini na moja! Philipo alikuwa na maarifa ya siri: alijua 'Yesu ni nani'!

Kuhudumiana mmoja na mwingine

Petro vile vile alisema ***"Mtu akihudumu na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu"*** **(1 Petro 4:11*).*** Paulo anatuonyesha kwamba Mungu anatuwezesha kuwa wahuduma "***Kwa Roho wa Mungu",*** kuwa tu wahuduma ***"wa mioyo"*** **(2 Wakorinto 3:3).** Maandiko yanasema ***"Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu*** [uweza] ***wetu watoka kwa Mungu, naye ndiye aliyetutoshelesha kuwa wahuduma wa agano jipya"*** **(aya 5-6).**

Huduma ambayo Petro anataja ni kuhudumiana mmoja na mwingine katika mwili:

- Kuna huduma ya neno [mausia ya Mungu]
- Kuna huduma ya masaidiano ambayo inazung umzia juu ya uhusiano katika huduma ya mwili.

Wakati tuna ufunuo wa siri, sio tu kwamba tuna uweza wa kuihudumu **siri ya ndani** na wandugu lakini tuna uweza wa kuingia kwenye ***ushirika*** wa siri, na tunafanya hayo kwa kuhudumiana mmoja na mwingine kama ***"Mawakili wazuri wa neema ya namna nyingi ya Mungu".***

Neema ya namna nyingi ya Mungu.

Hapana shaka kwamba Mungu katika neema yake anataka kanisa lake lipokee neema **ya namna nyingi.** Neema imekuwa ndio kitu kilichokosa katika huduma zetu na katika njia za maisha yetu. Wanadamu kila mara wanaona vyema kuishi kwa sheria na kwa hivyo kila kanisa

(dini au mwondoko) inaeleza vile wanaamini na vile washiriki wao wanastahili kufanya. Hata hivyo kanisa kama hilo linawaweka washiriki wao katika kutokomaa milele, bila kulishwa **hekima ya ndani** na kutokuhudumiwa **neema ya namna nyingi.** Inaonekana kuwa rahisi kwa viongozi kuweka sheria na kutaka watu watimize.

Hata hivyo kuna njia tofauti na ni kupitia kwa neema. Huduma ya neno na huduma ya uhusiano kwa mmoja na mwingine katika mwili inawezeshwa na kufanikishwa na inaweka huru na kujenga kwa neema ya Mungu sote tunapofanyika "***mawakili wema wa neema ya mamna nyingi ya Mungu".***

WAHUDUMA WA SIRI

Katika **Wakolosai 1:24-29** Paulo anatupa ufahamu wa ndani wa wito wake kuwa mhuduma. Kutoka haya tunajifundisha mambo yaliyo **ya muhimu** ya mhuduma wa kweli wa Kristo.

Wito wa kuteseka.

"*Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu, tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani kanisa lake"* Wakolosai 1:24.

Jambo la kwanza ambalo Paulo anasema kuhusu huduma yake ni kiwango cha mateso aliyopitia katika kutimiza mwito wake kuwa mhuduma kwa kanisa. Mateso haya yaliadhiri mwili wa Paulo. Ni mambo dhahili aliyoyapitia. Wengine wanavutwa kwa huduma kama kazi, kiteka uchumi, au cheo lakini mhuduma wa kweli wa Kristo kwanza anaitwa na mwito unahusisha mateso.

Yesu alisema ***"Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema hutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo"* Yohana 10:11.** Mhuduma wa kweli ni Yule '***Anatoa uhai wake kwa ajili ya wandugu'.*** Ni wito wa kuteseka**.**

Wahuduma wengine ni wa mshahara

Mtu ambaye anatafuta kwenda katika huduma kwa sababu za kibinafsi ni mtu wa mshahara. Yesu alisema humwona mbwa-mwitu anakuja, ***"yule hukimbia kwa kuwa ni mtu wa mshahara; wala mambo ya kondoo si kitu kwake"* Yohana 10:13.**

Maangalizi ya makanisa

Kuteseka kunakuja kwa kuubeba mzigo wa uwajibikaji kwa ajili ya mwili. Kwa kunakili ujuzi wa mateso aliyoyapitia katika shughuri za huduma yake, Paulo anasema kwamba kilicho mjia kila siku ilikuwa ***"Maangalizi ya makanisa yote"* 2 Wakorintho 11:28.** Paulo anasema mzigo wake mkuu sio mambo mazito aliyo **yapitia kimwili,** lakini maangalizi ya makanisa.

Ni mzigo wa maombezi

Paulo anasema mateso yake hakika yalikuwa ***"Mateso kwa ajili ya Kristo".*** Twajua Yesu alikuwa "***amepigwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa"* (Isaya 53:4)** na tunajua mateso yake na kifo ilikuwa ni ya kutulipia dhambi zetu kikamilifu. Paulo hayazungumzii haswa mateso ambayo Yesu alitubebea, lakini kuna wazo ambapo mhuduma anaweza kuingia katika mateso ya Kristo kwa maombi na maombezi, akijitambulisha na moyo wa Bwana kwa mwili wake. Kumbuka ya kuwa yale mateso Yesu aliteseka katika shamba la Gethisemane haikuwa ya kimwili lakini pengine ngumu kwake kuyachukua kuliko kuteseka kwa msalaba.

Kila mwafunzi wa kweli na kila mhuduma wa kweli lazima aje pahali pa **kustahimili** hata kama kuna ungumu, masubuko, mateso, na maumivu ya mwili, ***"Siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu"* 2 Wakorintho 4:8-10.** Tumeitwa kupitia mambo kama hayo kwa ajili ya mwili ili kuachilia neema katika mwili (**aya 15**).

Uwakili wa neema.

Huduma ni matokeo ya uweza wa neema. Mungu kupitia Roho Wake anatupa uwezo wa kuhudumu (**2 Wakorintho 3:5-6).** Paulo anasema kwamba ***"nimefanywa mhuduma wake,***

sawasawa na uwakili wa Mungu, niliopewa kwa faida yenu, nilitimize neno la Mungu"* (Wakolosai 1:25).** Uwakili huu ni wa neema. Paulo anasema katika **Waefeso 3:2-3** ya kwamba ilikuwa ***"uwakili wa neema ya Mungu aliopewa" kwa Paulo kwa ajili ya kanisa, ikimwezesha kuwa mhuduma wa neno ili kuujulisha ufunuo wa siri.

Wito wa kuhudumu unaweza kutimizwa tu ***"kulingana na karama ya neema ya Mungu"*** ambayo inamwezesha mhuduma kufanya kazi ya huduma – ni ***"kwa kadiri ya utendaji wa uweza wake"* (Efe 3:7)**

Huduma ya neno

Uwakili kutoka kwa Mungu ni ***"kulitimiza neno la Mungu"* Wakolosai 1:25.** Huduma tunayo zungumzia sio huduma ya mashemazi ambayo ni huduma ya kuhudumiana, lakini **ni huduma ya neno.** Mtume Petro aliiweka wazi kati ya wito wa kuhudumu neno na mwito wa kuhudumiana.

Katika **mdo 6:1-7** shinda ilionekana katika kanisa la Yerusalemu na jawabu ya mitume ilikuwa kuweka wahuduma wengine, ***"ili tuwaweke juu ya jambo hili; na sisi tutahudumu katika kuomba na kulihudumia lile neno".*** Matokeo ya mgawanyiko huu kazini ulikuwa ***"neno la Mungu likaenea na hesabu ya wanafuzi ikazidi sana".***

KUJUA NA KUZIHUBIRI SIRI

Ufunuo wa siri

Kulingana na maandiko **huduma ya neno** inatimizwa tu wakati mhuduma anaweza kuijuza ***"siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote" Wakolosai 1:26.*** Kimaandiko jambo la msingi la karama ya huduma ya mitume na manabii ni kupokea kutoka kwa Roho Mtakatifu ufunuo wa siri (**Efe 3:5)** na kufanya ijulikane na watakatifu. Kwa kalne nyingi huduma za mitume na manabii hazijakuwapo na kama zimekuwapo hazikupokelewa na kanisa. Kwa hivyo kanisa imekuwa na kutojua kwa ufahamu wa siri.

Hekima ya ndani

Siri ni hekima ya ndani ya Mungu na ni kwa wale ambao wamekomaa **(1 Wakorintho 2:6-7**). Inaweza tu kujulikana na wale ambao wamekomaa. Siri inajulikana tu kwa utendaji kazi wa huduma ya neno, ikiwaletea watakatifu ufunuo wa siri kupitia kwa Roho. Maarifa ya siri ndio njia ambayo Mungu anawapatia watakatifu urithi.

Urithi

Urithi ni ***"usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni… tayari kufunuliwa wakati wa mwisho"* 1 Petro 1:4-5.** Maarifa ya siri yanakuja kwa ufunuo na ufunuo huo unapatianwa kwanza na Roho kwa mitume na manabii. Diposa Urejesho wa mitume na manabii ni ya muhimu katika siku hizi ili kanisa lije katika utimilifu.

Utajiri wa utukufu

Maarifa ya siri ***"unajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa, nao ni Kristo ndani yenu tumaini la utukufu"* Wakolosai 1:27.** Ni maarifa ya siri inayojuza kupitia ufunuo utukufu wa Mungu. ***"Mungu aliiazimu tangu milele kwa utukufu wetu"* (1 Wakorintho 2:7).**

Ushirika wa siri

Paulo alineemeshwa ***"kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika. Na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote***

***ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote"* Efe 3:8-9.** Matokeo ya watakatifu kuja katika ufunuo wa siri ambao ni ushirika wa ndani, ni kwamba ***"hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho"* aya 10.**

Ushindi wa kanisa

Kwa hivyo ushindi wa kanisa juu ya maadui wa kiroho wa Mungu inategemea juu ya kanisa kuja katika maarifa ya siri na kwa hivyo tunahitaji wahuduma ambao wanaweza ***"kulitimiza neno la Mungu, siri ile"* Wakolosai 1:25-26,** kuleta ufunuo kwa watakatifu, kuwezesha kanisa lote kutembea katika ukomavu. Kutembea katika ukomavu ni kutembea katika utukufu na hii yote inategemea kanisa kuzijua siri. Kanisa inapokuja kujua siri na kutembea katika urithi, ***"dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa Yahweh kama maji yaifunikavyo bahari"* Habakuki 2:14.** Ushultani na nguvu zitashindwa na Babiloni itaanguka! (**Isaya 2:2-4. Mika 4:1-4**).

TUNAHUDUMU AJE?

"*Ambaye sisi tunamhubiri habari zake, tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo"* Wakolosai 1:28

Kuhubiri

Kuelezwa kwanza kwa huduma ya neno ni:

- Kumhubiri Kristo;
- Kulitangaza neno la Mungu;
- Kuhubiri "***Utajiri wake Kristo usiopimika"* Efe 3:8;**
- ***"Kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu"* Mdo 20:27*;***
- ***"Kuenenda ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe"* Mariko 16:15;**
- ***"Kuzihubiri habari njema za ufalme wa Mungu na jina lakeYesu Kristo"* Mdo 8:12.**

Kuonya

Neno hili '*Noutheteo'* Kiyunani inamaanisha: *kuweka kwa mawazo, kuonywa kwa njia ya upole* na inatafsiliwa 'onya, kujenga'.

Maelezo ya pili ya huduma ya neno ni:

- Kuonya kila mtu;
- ***"Kuonyana"*** mkiisha kujazwa na maarifa yote (**Warumi 15:14**);
- Wahuduma wapaswa kuwaonya watakatifu kama moja wapo wa njia ya kuwachunga (**1The 5:12**);
- Ambao hawalitii neno wanastahili kuonywa kama ndugu **2The 3:15**;
- Wakati neno la Mungu linadumu katika watakatifu wanaweza ***"kufundishana na kuonyana kwa zaburi na nyimbo na Tenzi za rohoni"* Wakolosai 3:16.**
- Maandiko yameandikwa kwa kutuonya sisi **1 Wakorintho 10:11**.

Kufundisha

Maelezo ya tatu ya huduma ya neno ni:

- Kumfundisha kila mtu;
- ***"Kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi"* Mathayo 28:20**
- Kuwafundisha ***"Mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu"* Ebr 5:12;**
- Kufundisha elimu ya Imani **Yuda 3**;

- Kufundisha mafundisho ya kitume **Mdo 2:42**;
- ***"Kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo"*** **Mdo 28:31;**
- ***"Hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo"*** **Mdo 5:42.**

Katika hekima yote

Maelezo ya nne katika huduma ya neno ni:

- Katika hekima yote;
- Kristo kwetu ni ***"hekima ya Mungu"*** **(1 Kor 1:24);**
- Kristo ***"alifanyika kwetu hekima itokayo kwa Mungu"*** (**1 Kor 1:30);**
- ***"Bora hekima"*** **(Mithali 4:7);**
- Ni hekima kutoka mbinguni **(Yakobo 3:17).**

Lengo ni utimilifu

"Kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo" **Wakolosai 1:28.**

Lengo la kazi ya huduma kwa kila mhuduma wa karama tano (**Efe 4:11)** ni ***"kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata na sisi sote…kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa kristo"*** **Efe 4:12-13.**

Mhuduma anawajibika kupitia huduma ya neno kuwaleta watakatifu kutoka kuwa watoto (**Efe 4:14)** kuwa watakatifu wakomavu, ambao wanaweza "***kushika kweli katika upendo" aya 15*** na kufanya kazi kikamilifu "***mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadri ya utendaji wa kila sehemu moja moja huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo"*** **Efe 4:16.** Lengo ni utimilifu: "***Tukaze mwendo tuufikilie utimilifu",*** tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ***"ya mausia ya Mungu"*** **Ebr 6:1.** atakatifu wastahili kuwa na ujuzi ***"katika neno la haki"*** **Ebr 5:13**. Hii itakuwa matokeo ya utendaji kazi uliofaulu wa huduma ya neno.

Huduma ni *"kulingana na utendaje wake"*

"Nami najitaabisha kwa neno lilo hilo, nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu" **Kol 1:29.** Mhuduma ameitwa ***"Kutaabika"*** na kujitahidi katika kazi ya huduma. Mhuduma anastahili ***"kujitahidi kujionyesha kuwa amekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari ukitumia kwa halali neno la kweli"*** **2 Timotheo 2:15.**

Hata hivyo jambo kuu katika huduma ni kujua ***"Utendaji kazi wake"*** ndani yetu; ni utendaji kazi wa Mungu, **nguvu za utendaji kazi** zikifanya kazi ndani yetu na kupitia sisi. Huduma ya kufaulu ni Mungu akifanya kazi ndani yetu kwa nguvu zake akileta matokeo yanayoonekana.

"Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawezayo kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu" **Efe 3:20.** Jawabu ya ombi la ajabu la Paulo kwetu ili ***"kufanywa imara kwa nguvu" aya 16;*** ili mioyo yetu ijawe na imani na kwamba tupate kuelewa upendo wake na tujawe ***"Na utimilifu wote wa Mungu"*** **(aya 17-19)** inawezekana tu kwa kuwa tu wana wa Mungu – nguvu zake tayari zinafanya kazi ndani yetu.

Ni kazi hiyo hiyo ambayo inafanya kazi ndani ya mhuduma, ikimwezesha mhuduma "***kumuwakilisha kila mtu mkamilifu katika Kristo Yesu".***

SIRI YA UTAUWA NI KUU!

1 Timotheo 3:15 inasema kwamba ***"kanisa ya Mungu aliye hai ni nguzo na msingi wa kweli"***. Nguzo ya muhimu ya kweli ambayo yatakikana ieleweke na ihimizwe katika kanisa ni ukweli kuhusu siri ya utauwa.

> ***"Na bila shaka siri ya utauwa ni kuu. Mungu alidhihirishwa katika mwili, akajulikana kuwa na haki katika Roho, akaonekana na malaika, akahubiriwa katika Mataifa, akaaminiwa katika ulimwengu, akachukuliwa juu katika utukufu"*** **1Timotheo 3:16.**

Siri ya utauwa ni **bila shaka.** 'Bila shaka' ni neno la Kiyunani *homologoumenos,* inamaanisha kwa kukiri na inatoka kwa neno *homologeo* ikimaanisha 'kukiri' au 'kuongea jambo moja'. Siri hii inatakiwa kukiliwa kwa kweli na ujasiri wa ndani katika ukweli wake na hakuna ubishi ambao unaweza kusimama kinyume chake. Kukiri kwetu ni kukubaliana na ukweli wa siri hii kama ilivyo funuliwa na neno la Mungu.

SIRI YA UTAUWA

Mungu alidhihirishwa katika mwili

Mungu alifanyika mtu! "*Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuweko kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu" Yohana 1:1. "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli"* aya 14. Yesu ndiye **Neno la Mungu;** hiyo ni moja wapo ya jina lake katika **ufunuo 19:13.**

Yesu alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili!

Katika **1Yohana 1:1-3,** Yesu ameelezwa kama "***Lile lililokuwako tangu mwanzo" na "Neno la uzima",*** na hisia tatu za kawaida zinatumika katika maelezo: **Kusikia, "*Tulilolisikia,"* Kuona, "*tuliloliona kwa macho yetu",* Kuguza, *"na mikono yetu ikalipapasa".*** Yohana anatutangazia kwamba "***Uzima huo ulidthihirika" aya 2.*** Mungu alidhihirishwa katika mwili na mashahidi walisikia, waliona na wakamguza!

Paulo akiwaandikia **Wafilipi** kuhusu Kristo Yesu ananena kumhusu "***ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu***…" **Wafilipi 2:6-8a.** Mungu alikuja kwa mfano wa wanadamu na akaonekana akiwa na mfano wa mwanadamu! Paulo anaandika ***"Mtu wa kwanza atoka katika nchi, ni wa udongo. Mtu wa pili atoka mbinguni"*** **1 Wakorintho 15:47.**

Mungu alifanywa haki katika Roho

Mungu, ambaye **alidhihirishwa** katika mwili pia **alifanywa haki** katika Roho. Neno hili *dikaioo* linamaanisha 'kufanya haki au bila kosa'. Mungu aliyedhihirishwa katika mwili alishuhudiwa, au akafanywa haki au bila kosa, na Roho Mtakatifu.

Yohana anafundisha juu ya kujaribu maroho. Anasema ***"katika hili mwamjua Roho wa Mungu; kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kira roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu. Na hii ndiyo roho ya mpinga Kristo"*** **1 Yohana 4:2-3a.** Kukiri kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili ni **Kufanywa haki katika Roho!**

Roho Mtakatifu anamfanya Yesu haki kama Mwana wa Mungu

- **Katika kupatikana kwake.** Malaika aliyenena na Mariamu alisema "***Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu Mwana wa Mungu"*** **Lk 1:35.**

- **Katika ubatizo waYesu,** Roho Mtakatifu **alimfanya haki** kuwa **Mwana wa Mungu,** "***Naye yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia akamwona roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye"*** **Mathayo 3:16-17.**

- **Kupitia kufufuka kwake**, ***"Yaani, habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili, na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu"*** **Warumi 1:3-4**

Mwana wa Mungu ni nani?

Mwana anaelezwa kama ***"Mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake"*** **Ebr 1:3;** ***"Mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote"*** **Kol 1:15**; Kristo ni ***"Sura yake Mungu"*** na "***Nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo"*** **2 Kor 4:4, 6. Mwana wa Mungu ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili katika mtu Yesu Kristo. Yesu alifanywa haki katika Roho Kama Mwana wa Mungu!**

Alionekana na malaika

Yesu katika hali nyingi **alionekana na malaika:**

- Malaika walitangaza Yesu kama Mwana wa Mungu wakati wa kupatikana kwake. ***"Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako … hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu Mwana wa Mungu"*** **Lk 1:35.**

- Malaika walikusanyika katika kuzaliwa kwake, ***"Malaika wa Bwana akawatokea ghafla… malaika akawaambia msiogope … maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa kwa ajili yenu Mwokozi, ndiye Kristo Bwana"*** **Lk 2:9-13.**

- Malaika walimhudumia baada ya kujaribiwa kwake jangwani, ***"Kisha ibilisi akamwacha na tazama, wakaja malaika wakamtumikia"*** **Mt 4:11.**

- Malaika pia alimhudumia katika shamba la Gethsemane wakati alijipatiana kwa mapenzi ya Baba, ***"Malaika kutoka mbinguni akamtokea akamtia nguvu"*** **Lk 22:43**

- Malaika walidhibitisha kufufuka kwake kwa baadhi ya wanawake waliokuja katika kaburi na wasipate mwili wa Bwana Yesu, ***"Ikawa walipokuwa wakifadhaika kwa ajili ya neno hilo tazama, watu wawili walisimama karibu nao wakivaa nguo za kumeta meta nao walipoingiwa na hofu na kuinama kifundifundi hata nchi, hawa waliwaambia, kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? hayupo hapa, amefufuka"*** **Lk 24:4-6.**

- Malaika walikuwa na Yesu kushuhudia kupaa kwa Yesu mbinguni, ***"Walipokuwa wakitazama akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. Walipokuwa***

wakikaza macho Mbiguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wakasema, enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni **Mdo 1:9-11.**

Alihubiriwa katika Mataifa

Mungu, ambayo alidhirishwa katika mwili ndani ya Yesu, pia amehubiriwa katika Mataifa. **Mariko** anashuhudia kwamba mitume "***Wakatoka, wakahubiri kote kote Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulidhibitisha kwa ishala zilizofuatana nalo"*** **Mk 16:20.**
"***Wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno"*** **Mdo 8:4.**

Paulo alimshuhudia Timotheo juu yake kwamba "***naliwekwa niwe mhubiri na mtume… mwalimu wa Mataifa katika imani na kweli" 1Tim 2:7.*** Paulo aliihubiri siri ya utauwa kama alivyopewa neema ***"kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika"*** **Efe 3:8.** Paulo alikuwa mtume wa Mataifa (**Gal 2:7-8)** na alitumika sana katika siri hii **ikihubiriwa katika Mataifa.**

Paulo, katika Efeso ***"Alihojiana na watu kila siku"*** katika shule ya Tirano kwa miaka miwili. Matokeo ya haya yalikuwa ***"wote waliokaa Asia*** (Turkey na maeneo yaliozingira) ***Wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani"*** **Mdo 19:9-10.**

Paulo, akiwaandikia **Wathesalonike** anawashuhudia kwamba, ***"kutoka kwenu neno la Mungu limevuma… kila mahali"*** **1 The 1:8.** Kwa **Wakolosai** anasema kwamba **"*neno la kweli ya injili … iliofika kwenu, kama ilivyo katika ulimwengu wote"*** **1 Kol 1:5b-6.**

Siri hii ya utauwa, ambayo Mungu amedhihirishwa katika mwili,
hakika imehubiriwa kwa Mataifa!

Aliaminiwa duniani

Katika **Mdo 8:35-37** Philipo ***"akamhubiri Yesu"*** kwa Towashi wa Kushi. Baada ya kuyasikia mahubiri, kukiri kwake kulikuwa, ***"Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu"*** **aya 37.** Kama vile Kolinelio na watu wengine wa Mataifa ambao walikuwa wamekusanyika walisikia neno likihubiriwa na Petro, ***"kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi",*** juu yao "***Roho Mtakatifu akawashukia"*** **Mdo 10:43-44.**

Waefeso waliamini vile Paulo alihubiri, "***Nanyi pia katika huyu mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa mhuri na Roho Yule wa ahadi aliye Mtakatifu"*** **Efe 1:13.**

Yule mlinzi wa gereza na nyumba yake waliokoka "***kwa kuamini Bwana Yesu Kristo"*** **Mdo 16:31-32.** Hata leo watu wanamwamini Bwana Yesu Kristo na wanaokolewa.

Kupokelewa juu katika utukufu

Tukio la ajabu la Yesu **kupokelewa juu katika utukufu** lilishuhudiwa na mitume, "***walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao"*** **Mdo 1:9.**

Yesu alisema, ***"Ndipo itakapoonekana ishara yake mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi"*** **Mt 24:30.** Yesu alipokelewa juu katika utukufu na atakuja vivyo hivyo!

Stefano alikuwa na ufunuo wa Yesu **kupokelewa juu katika utukufu** wakati alipotangaza "***Tazama! Naona mbigu zimefunguka, na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa Mungu"*** **Mdo 7:56.**

Yesu ***"Akiisha kufanya utakaso wa dhambi aliketi mkono wa kuume wa ukuu huko juu"*** **Ebr 1:3.** ***"Alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu"*** **Ebr 6:19-20.**

Kwa kukiri bila shaka, huyu Yesu, ambaye ni Kristo, ndiye Mungu aliyedhihirishwa katika mwili na akapokelewa juu katika utukufu!

Hii ni siri kubwa ambayo inastahili kukiriwa kwa uhakika:

- **Mungu alidhirishwa katika mwili,**
- **Akajulikana kuwa na haki katika Roho,**
- **Akaonekana na malaikas,**
- **Akahubiriwa katika mataifa,**
- **Akaaminiwa katika ulimwengu,**
- **Akachukuliwa juu katika utukufu!**

KUGEUZWA KWA WATAKATIFU

Kugeuzwa

*"**Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe (**metamorphoo**) kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema ya kumpendeza, na ukamilifu"*** **Rom 12:1-2**

Tambua kwamba jina 'kugeuzwa' ni jina moja na jina la Kiyunani ambalo limetafsiriwa 'kubadilishwa' (**Mt 17:2**). Yesu alibadilishwa mbele ya wanafunzi wake watatu. Kuonekana kweke hata mavazi yake yaligeuzwa, hivyo ni, **kubadilishwa katika hali ingine,** kubadilishwa, na katika, utukufu wa Mungu. Lengo la Mungu kwa watakatifu ni kuwa kama Yesu: kubadilishwa kutoka kwa mwili wa asili mpaka kwa mwili wa utukufu.

Neno hili la Kiyunani *Metamorphoo* linatumika tu sehemu tatu katika agano jipya katika **Warumi 12:2** hapo juu, katika maandiko ambayo yanazungumzia kubadilishwa kwa Yesu katika Injili na katika **2 Wakorintho 3:18** ***"Lakini sisi sote kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana aliye Roho."***

Kufanywa upya nia

Katika **Warumi 12:12 tunageuzwa kwa kufanywa upya nia zetu.** Nia zetu zinafanywa upya kupitia toba, 'kule kugeuzwa nia kwa kwanza' kuamini injili na kuendelea kuzitubia "***kazi zisizo na uhai"*** sio kufungwa na mawazo ya dini**.**

Nia zetu zinafanywa upya na ufunuo wa maarifa ya neno, kwa kuwa ***"macho ya mioyo yetu tatiwe nuru"*** **Efe 1:18.** Kugeuzwa katika mahali ambapo tunajua na tunaweza kuyafanya mapenzi ya Mungu inahitaji ***"mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu mpya ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli"*** **Efe 4:23-24**

Kuabudu katika roho na kweli

Kugeuzwa ambako kunatajwa katika **2 Wakorintho 3:18** ni kwa ***"Roho wa Bwana***". Hii inazungumzia kugeuzwa kwa kiroho ambako kunatendeka tunapomuabudu Bwana ndani na kwa Roho. Yesu alisema kwamba ibada ya kweli ni "***katika roho na kweli"*** **Yohana 4:24.** Kuabudu katika roho ni: Roho anatuwezesha kupata Mungu na kupatikana katika utukufu wake katika ibada. Kuabudu katika kweli ni matokeo ya kulipokea neno kwa ufunuo kupitia kuwa na roho za nia yetu zikifanywa upya ili tulipokee neno kwa ufunuo.

Lengo la Mungu kwetu ni ***"kufananishwa na mfano wa Mwana wake"*** **Rom 8:29,** hivyo ni, kuwa kama Yesu. Yesu alikuja pahali katika ukomavu wake ambapo aliweza **kubadilishwa.** Kupitia kugeuzwa tutakuja pahali pale tunapotembea katika ukomavu.

Wandugu, kugeuzwa huku kunatendeka. Ufufuo wa siku za mwisho ambao unatutayarisha kuwa ***"kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo…takatifu lisilo na mawaa"*** **Efe 5:27** ambalo Yesu atajiletea atakapokuja, kumeanza. Ni kuachiliwa na ujuzi wa neema Yake ambao unatendeka!

Kwa neema kuachiliwa kupitia ukombozi

Neema hii imepatianwa kwetu katika Kristo Yesu Kabla ya nyakati kuanza lakini sasa inakuwa hakika katika ujuzi wetu (**2 Timotheo 1:9-10**). Kama tujuavyo Yesu alikamilisha kazi ya ukombozi kikamilifu kupitia msalaba na kuingia kwake mbinguni na damu yake mwenyewe. Kupitia yeye tumefanywa haki lakini pia tumetukuzwa (**Rom 8:30**) na ni kwa kuingia katika utukufu ambako Mungu anafanya iwezekane leo kupitia ufunuo wa siri "***Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu"*** **Kol 1:27** na kwa kufanya ijulikane hekima ya ndani ya neno lake *"**ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu"*** **1 Kor 2:7.**

Neema

- **Inatufanya haki – "*Ili tuhesabiwe haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu"*** **Tito 3:7**
- **Inatuwezesha kufanya kazi katika mwili –** tumepewa karama kulingana na neema hii kutuwezesha kufanya kazi katika mwili katika unabii, kufundisha, huduma, kuonya, kuongoza, kukilimu na kurehemu (**Warumi 12:6-8**).
- **Inahudumu kupitia huduma tano – "*Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo"*** **Efe 4:7.** Kipawa ni karama tano. "***Alipopaa juu aliteka mateka akawapa wanadamu vipawa – naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu"*** **Efe 4:8, 11.** Karama hii ya huduma inafanya kazi kwa neema kwa "***kuwakamilisha watakatifu" [***kutayarisha – kuweka mwili katika mpangilio ili kila mtu aweze kufanya kazi kwa uhuru na kikamilifu]. Huduma hizi zinapoinuliwa na kupokelewa katika mwili basi mwili wote utajengeka mpaka sisi wote tutakapoufikia utimilifu (**Efe 4:12-13**).

Sisi washiriki wa mwili wake

Ni wakati wa watakatifu kuona na kufahamu kwamba kuna **mwili mmoja** na Mungu amechagua pahali pa kila mmoja wetu katika mwili na ya kuwa Mungu ametufanya kila mmoja kuwa mshiriki wa mwili wake, akichagua karama za huduma mbalimbali, kwa uongozi (**1 Wakorintho 12:18, 28**), na karama zote zingine ambazo zinajenga na kuwezesha kanisa kufanya kazi kikamilifu katika upendo wa Mungu, zikionyesha upendo huo kwa ulimwengu (**1 Wakorintho 13:4-8**)

Urithi

Ufufuo umeanza na watakatifu binafsi wakihusisha wahuduma wana:

a) Wanapokea neema kubwa ambayo inawaleta katika uhakika wa kufanyika wana,
b) Ufahamu 'kuwekwa pahali pako' ambayo Mungu anawapatia wana wake ambao wamekomaa kuwa watumishi wake,
c) Wakitende kazi kikamilifu kama wana,
d) Wakitembea katika urithi.

Mungu ametukilimia "***urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu uliotayari kufunuliwa wakati wa mwisho"*** **1Pet 1:3-5.**

Urithi umehifadhiwa mbinguni lakini inastahili kupokelewa duniani siku za mwisho. ***'Wakati'*** hapa ni *'Kairos'* ikimaanisha wakati wa neema ambayo Mungu anafanya kazi maalum

kwa watu wake; '*kairos'* inazungumzia yale ambayo yanatendeka katika nyakati za mda; Petro anazungumzia nyakati kutoka sasa hadi kurudi kwa Bwana.

Ni kulingana na kuwekewa hatima

Tumewekewa hatima yetu kama wana na Yesu Kristo mwenyewe:

- Nikulingana na mapenzi yake mema, kwa sifa za utukufu wa neema yake (**Efe 1:5-6**)
- "***Kufananishwa na mfano wa Mwana wake"*** **Rom 8:29 –** hii huja kwa kufanywa wana ambapo tunawekwa kama wana.
- Tunakuwa kama wana tukineemeshwa kutembea katika ukomavu tukimjua Baba kwa undani kuliko mwanzo.
- Kuongozwa na Roho kama wana (**Warumi 8:14**)
- Mungu anawaleta wana wengi kwa utukufu kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso (**Ebr 2:10**)
- Viumbe vyote vinangojea kufunuliwa kwa wana (**Rom 8:19**)

Ni nani anaweza kuingia kwenye ufufuo huu?

Ufufuo ni kupokea Roho wa kufanywa wana. Watoto wa Mungu wote wamewekewa kukua kufanyika wana.

Tunafaulu jinsi gani kufanyika wana?

Kizazi chote cha watu ambao Mungu alikomboa kutoka Misiri waliwekewa kuingia katika nchi ya ahadi. Ilikuwa ni Mungu aliwakomboa kwa kuyagawanya maji ya bahari ya Shamu; ilikuwa ni Mungu aliwaleta kupitia njangwa kuja kwa Mlima Sinai. Maandiko yanasema, "***Niliwachukua ninyi juu ya bawa za tai"*** **Kutoka 19:4.** Aliwaleta watu kwa mlima Sinai, kwa mlima mtakatifu, kuwapa sheria – **Pasaka ya kwanza.**

Alituokoa kutoka kwa ulimwengu kwa damu ya Yesu na akatuleta katika Kristo kupitia ubatizo, akitumwagia Roho wake Mtakatifu - **pasaka ya pili** na kutimizwa kwake; lakini sasa anataka sisi tuje katika nchi ya urithi, hatimaye kuja kwake katika Sayuni na kuishi mbele yake kikamilifu. Haya ndiyo matokeo ya kupokea Roho wa kufanyika wana; kupokea roho wa wana ni tukio la kubadilishwa ambayo inatuelekeza katika utukufu wa Baba, ikituwezesha kutembea kama wana, tukifanywa upya katika nia ya roho zetu.

Tunaingia kwa imani

Amefanya maagano nasi hata kama vile alifanya maagano na Musa na wana wa Israeli. Wakati walivuka njagwa na wakafika Kadesh- barnea, hawakuwa watu waliokamilika; walikuwa kikundi kilichochanganyika – watoto wao walikuwa nao. Ndio wale wale ambao walimfanya Haruni atengeneze dama wa dhahabu na **kama wangemwamini Mungu, wengeingia mji hapo hapo, wakati uo huo.** Ilikuwa ni kutoamini kwao kuliko waelekeza katika kuasi kwao na wakakataa kuingia – walikataa urithi ulioahidiwa.

Lakini miaka arubaine badaye watoto wao (wana wao) walirithi. Hivyo ndivyo ilivyo kwa watu wa Mungu leo: Ni kwa njia ya imani ambapo tunaingia katika urithi ambao Mungu ako nao kwa ajili Yetu. Na imani huja kwa kusikia **Rom 10:17**. Ni wakati tunasikia neno kuhusu uwana, kuhusu kuwekwa pahali pako; kuhusu kuachiliwa kwa neema, ambapo tunawezeshwa kutembea katika urithi. Tunaingia katika urithi wetu kwa njia ya imani. Sio kwa kazi ni kwa wakati uliokwisha kuamuriwa na Baba **(Wagalatia 4:2).**

Lengo ni utukufu

Katika **Wakolosai** Paulo anatamatisha 'siri': ***"Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu".*** Mungu anakusudia kufunua utukufu wake ulimwenguni kupitia watu wake. Ni kwa sababu ya neema ambapo Paulo aliweza "***kuwahubiri mataifa utajiri wake Kristo usiopimika na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote; ili sasa kwa njia ya kanisa hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho"*** **Efe 3:8-10**

i. Ni kupitia kanisa ambapo Mungu anafunua ushindi kamili wa Kristo ulimwenguni;
ii. Ni kwa kanisa ambalo limekomaa;
iii. Ni kupitia Roho Mtakatifu akiwainua mitume na manabii ambao wanaweza kuleta maarifa ya siri;
iv. Ni kwa kanisa ambalo limesimama imara katika wakati wa mateso wakati upinzani wote, ikihusisha pia mateso ya moja kwa moja, inapatikana.

Mungu aliahidi kwamba yeye, Mungu wa neema yote "*atawatengeneza, na kuwadhibitisha na kuwatia nguvu"* 1Petro 5:10.

SEHEMU NNE ZA NEEMA – SEHEMU MBILI UKWELI

Neno lilifanyika kuwa mwili

Neema na kweli

"*Naye neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli"* Yohana 1:14.

Ufunuo wa utukufu wa Mungu ni **neema** na **kweli!** Huu ni ufunuo! Wengi wameuweka utukufu katika kuja kwa Kristo, au tutakapo kwenda mbinguni. Wengine wamefikiria kwamba utukufu ni uthihirisho wa 'mavumbi ya dhahabu' yakishukia miili ya wanadamu.

Yesu ni wa milele

Hata hivyo ufunuo wa utukufu ni ndani ya Yesu aliye Masihi na ufunuo huo ***"umejaa neema na kweli".*** Katika **aya 15** Yohana anasema kwamba Yesu ***"Ajaye nyuma yangu amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu".*** Yohana anazungumza juu ya Yule wa milele, ambaye alifanyika mwili. Yesu alisema ***"Amin, amin, nawaambia, Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO"* Yohana 8:58.** Wakati askari walikuja kukamata Yesu katika shamba aliwauliza ***"Ni nani mnayemtafuta? Wao wakamjibu ni Yesu Mnazareti. Yesu akawaambia, NI MIMI"* Yohana 18: 4-5.** Tambua ya kwamba Yesu alisema "***NI MIMI"***. Kama matokeo ya kukiri kwa Yesu kuwa yeye ni nani, utukufu na nguvu kwa mda zilithihirika na "***walirudi nyuma wakaanguka chini"* aya 6.**

Neema juu ya neema

"*Kwa kuwa katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema"* Yohana 1:16. Hili ni andiko la ajabu na wengi wamekosa ufunuo wa neema ya Mungu katika Kristo aliye Masihi. **Neema juu ya neema,** neema mara mbili! Neema ikiongezeka! Kila mara kuna neema nyingi inayopatikana.

Kiti cha neema

Kiti cha enzi cha Mungu ni **KITI CHA NEEMA (Ebr 4:16).** Katika kiti cha enzi cha neema tunapokea ***"rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji".***

- **<u>Twahitaji rehema kufunika maisha yetu ya kale.</u>**
- **<u>Twahitaji neema kwa leo na kesho.</u>**

Roho wa neema

Roho wa Mungu ni **ROHO WA NEEMA (Ebr 10:29, Zakaria 12:10).** Roho wa neema anaitwa pia Roho wa dua na ni Roho anayetusaidia kuomba na kufanya maombezi (**Rom 8:26-27**). Ni Roho wa neema ambaye anatuleta katika ufahamu wa Mwokozi wetu na kifo Chake na ufufuo.

Tunaishi kwa neema

"Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo"* Yn 1:17.** Yesu alikuja kutimiza torati na kutimizwa kwa torati ni kuachiliwa/ kudhihirishwa kwa **neema** na **kweli.** Hatupo tena *"**chini ya sheri, bali chini ya neema" **(Rom**

6:14) na "***tumehesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu"*** **Rom 3:24.**

Neema hata juu ya kweli

Katika **Yohana 1:14, 16, na 17, NEEMA** imetajwa mara nne na **KWELI** imetajwa mara mbili: **neema** sehemu nne**, kweli** sehemu mbili. Wakati Mungu alifanyika mwanadamu katika Yesu ambaye ni "***Mwana pekee atokaye kwa Mungu"*** **aya 14,** huyo ni, Yesu udhihirisho wa Mungu katika mwili, alifunuliwa katika neema na kweli, lakini neema inahimizwa hata juu ya kweli. Huu ni ufunuo wa ajabu ambao Mungu anauleta kwa kanisa lake siku hizi.

Roho wa uwana inaachilia neema

Mwondoko wa 'kiroho' uliitwa 'wa kiroho' na hii haswa inazungumzia 'karama ya neema'. *Charis* ni jina la Kiyunani la neema. Tunamshukuru Mungu kwa sababu ya mwondoko wa kiroho ambao umerejesha ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuachiliwa kwa vipawa tisa vya Roho (**1Kor 12:6-11**) kwa mamilioni ya waamini ulimwenguni kote na ikaingia ndani ya dini nyigi za kitamaduni za kikristo na kufanywa upya na ufufuo. Hata hivyo, himizo katika mwondoko wa kiroho ulikuwa zaidi juu ya karama, upako na huduma ya nguvu na ndio hayo yote ni halali lakini uhakika wa neema ya Mungu ulikuwa kamwe haujajulikana. Hakika ni utendaji kazi unao endelea sasa wa Roho Mtakatifu katika kulileta kanisa katika uhakika wa kufanywa wana na Roho wa uwana (kuwekwa pahali pako) ambapo tunakuja kujua uhakika wa neema ya Mungu.

Uhakika wa neema

1) Inapatikana kwa imani

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi yenu, ni kipawa cha Mungu" **Efe 2:8.** Neema imepatianwa na Mungu "***katika Kristo Yesu tangu milele"*** **2 Tim 1:9,** lakini kwanza imepatianwa kwetu tunapokuja kwa imani ndani ya Yesu Kristo Mwokozi wetu. Kwa hivyo funguo za neema ni **imani.** Neema imepatianwa na Mugu kwa kuwa neema ni kumwagwa au uthihirisho wa asiri ya Mungu – utukufu wake ***"umejaa neema",*** na utukufu wake unadhihirika ndani ya mtu Yesu Kristo. Tunapokea neema ya bure isio na kipimo ya Mungu kwa imani, kwa kumwamini Yesu aliye Masihi na ya kwamba alifia dhambi zetu na akafufuka tena kulingana na maandiko.

2) Tunakua katika neema

Petro anasema ***"Kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo"*** **2 Pet 3:18.** ***"Kwa kuwa alitangulia kutujua ili tufanywe wanawe…usifiwe utukufu wa neema yake ambayo ametuneemesha katika huyu mpendwa"*** **Efe 1:5-6.** Kupokea roho wa uwana inatuwezesha kukua zaidi katika neema ya Bwana wetu na Mwokozi wetu na kukombolewa **"*sawasawa na wingi wa neema yake"*** **Efe 1:7.** Urithi tunaoupokea kama wana ni neema kuu ambayo inatuwezesha kutembea katika Roho na kwa hivyo ***"Kuongozwa na Roho wa Mungu"*** kama wana wake (**Rom 8:14)**.

3) Neema inatuwezesha kusimama

"*Ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo tunasimama ndani yake, na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu"* **Rom 5:2.** Mara tena imani ndio kiingilio cha neema na kupitia imani ndani ya Yesu Kristo tunakuja katika msimamo ndani ya neema. Neema inatuwezesha ***"kufurahia katika tumaini la utukufu wa***

Mungu" lakini pia ***"tufurahi katika dhiki"*** **aya 3.** Kanisa la sasa limefanyika dhaifu na mafundisho ya uongo wa nyakati na ahadi kwamba wakristo watanyakuliwa toka ulimwenguni kabla ya dhiki kuu kutendeka. Mafundiso kama hayo hayana uhakika ukianagalia historia ya Nazism na Communism katika karne ya ishirini na maovu kama yale yaliotokea Rwanda ya mwaka wa 1994. Hata hivyo jambo kuu lililokosa katika mafundisho ya kanisa imekuwa ni kupuuza kwa neema ya Mungu, kwamba hakika ni neema ambayo inatuwezesha "***kufurahi katika dhiki".***

4) Neema inaweza kuonekana

"Naye alipokwisha kufika na kuiona neema ya Mungu akafurahi, akawasihi wote waambatane na Bwana kwa kusudi la moyo" **Mdo 11:23.** Baranaba **angeiona neema ya Mungu** katika kanisa Jipya la Antiokia. Neema hii ilikuwa imewawezesha wanafunzi kutoka Yerusalemu kuwaleta Wayahudi na Wayunani pamoja kanisani mara ya kwanza katika historia ya kanisa: neema kuu jinsi gani! Maandiko yananena juu ya kanisa la kwanza la Yerusalemu, ***"Neema nyingi ikawa juu yao wote"*** **Mdo 4:33.** Mitume waliwahimiza waamini wapya katika Antiokia Pisidia, wakiwasihi ***"kudumu katika neema ya Mungu"*** **Mdo 13:43.** Neema inaonekana ikienea kupitia wengi ikisababisha ***"Shukrani izidishwe na Mungu atukuzwe"*** **2 Kor 4:15.** Mitume viongozi katika Yerusalemu "***walipokwisha kuijua ile neema iliyopeanwa"*** kwa Paulo na Baranaba (**Wagalatia 2:9**). Alama ya neema ya mtume na wahuduma wote wa karama tano ni kwamba neema inaonekana katika maisha yao na wanaihudumu.

Unyenyekevu – funguo za neema

"*Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema"* **1 Pet 5:5, Yakobo 4:6.** Unyenyekevu unaonekana katika utiifu, kwanza utiifu kwa Mungu na pili utiifu kwa mmoja na mwingine. Mtu mnyenyekevu hakika atapokea neema nyingi. Mazingara ambayo tunapokea neema kupitia unyenyekevu ni kwa kuwa mtu mtiifu katika mwili wa Yesu Kristo.

Katika kipindi cha nyuma utiifu ulifundishwa vibaya kama kuwa watiifu kwa mamlaka. Utiifu wa kweli ambayo ni kazi ya neema katika maisha yetu ni zaidi kuliko kutii mamlaka; hakika ni kunyenyekeana katika mwili ***"Katika kicho cha Kristo"*** **Efe 5:21,** na utiifu kama huo ni ishara ya maisha yaliojaa Roho **Efe 5:18-21**.

Utiifu kwa Mungu na kwa mmoja na mwingine katika mwili ni ishara ya mtu mnyenyekevu na kwa hivyo kazi kuu ya neema katika maisha ya mtu huyo. Mwili hautafanya kazi vizuri mpaka tutakapopata neema kuu ambayo inadhihirika katika utiifu wa kweli kwa Mungu na kwa mmoja na mwingine tunapotembea katika unyenyekevu.

Neema – funguo za huduma

"Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu" **1Pet 4:10.** Karama zote zilizonakiliwa katika **Warumi 12:6-8, 1 Kor 12:8-10** na katika **Efe 4:11** ziko katika mazingira ya neema na hivyo zinaweza kuitwa **karama za neema.** Hata hivyo katika kufuatilia karama na kuzifanyisha kazi, mwelekeo huu wa neema mara kwa mara umepuuzwa.

Tunatakiwa tuwe **mawakili wema** wa neema ya Mungu. Paulo anasema ilikuwa ***"neema ya Mungu"*** **Efe 3:2** ambayo ilimwezesha kuhudumu, haswa kufanya zijulikane siri. Anasema alifanyika ***"mhudumu wake, kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu"*** **aya 7** na ***"nalipewa neema hii ya kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo Usiopimika"*** **aya 8.**

Kila karama ya huduma inawezeshwa na kufanyishwa kazi katika neema na inatakiwa kuwa kielelezo cha **neema ya namna nyingi** ya Mungu. Tunapohudumu katika neema kutakuwa na shukrani zikimuendea Mungu, tukimpa utukufu katika Kristo Yesu.

Kuzungumza neno na kuhudumu katika uhusiano

***"Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu"* -** mausia yanazungumzia 'pahali pa Mungu pa kunenea' na inaongea juu ya Mungu akiongea kutoka patakatifu pa patakatifu, **Kutoka 25:22**. ***"Mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina"* 1Pet 4:11.**

Karama inaonekana kwa njia mbili: **kusema na kuhudumu.** Kusema inazungumzia kuhudumu kwa neno, lakini kuhudumu inamaanisha kufanya kazi kama shemazi, kungojea mezani, kuwa mtenda kazi. **Kuhudumu** inaongea juu ya vile tunatumikiana mmoja kwa mwingine na ndio funguo ya kujenga uhusiano wa kiungu wenye afya, mkamilifu katika mwili wa kristo –kwa kuhudumiana mmoja na mwingine.

Neema na utume.

Mambo mawili ya muhimu katika urejesho wa kitume ni: ufunuo wa siri {huduma ya neno} na kujenga uhusiano katika mwili. Yote haya mawili yanawezekana tu kupitia kuachilia na ujuzi wa neema. Paulo anasema ***"Katika yeye tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani, kwa ajili ya jina lake"* Rom 1:5.** Utume katika mazingira haya yanazungumzia kutumwa ambako Yeu amepeana katika **Mt 28: 19-20** kwa mitume wake kufanya wanafunzi kwa Mataifa yote. Jambo kuu la utume ni huduma ya neno (**Mdo 6:4**) walakini bila neema, huduma ya neno inakua na uhitaji (kisheria) ikileta hukumu na utumwa badala ya kuwaachilia watakatifu katika uhuru wa Masihi.

Ninaamini ya kwamba Mungu anatamani tupate huu ufunuo wa neema. Bila neema mitume pude wanafanyika viongozi wa kikundi kingine. Neema ni kila kinachowezesha 'utume' na karama zote za huduma hakika kufaidi na kujenga mwili kuwa "***mtu mkamilifu"* Efe 4:13.**

Agano jipya

Yesu ndiye mpatanishi wa agano jipya na hiyo agano inapatianwa kwetu kupitia kifo na kufufuka kwake. Kupitia Yesu utukufu wa Mungu sasa unaweza kudhihirishwa katika ulimwengu kupitia kanisa. Na Mungu akifanyika mwanadamu katika Mwana, Yesu, utukufu wa Mungu unafunuliwa uwe **umejaa neema na kweli.** Katika ufunuo wa Mungu ndani ya Kristo, Mungu anafunuliwa kuwa **NEEMA sehemu nne na KWELI sehemu mbili.**

Tumekuwa hatujasawasika kwa karne nyingi. Tangia kufanya upya kwa karne ya kumi na sita kumekuwa na kukua kwa uhimizo juu ya **kweli ["*neno lako ndiyo kweli"* Yn 17:17**] na neno limehubiriwa kwa nguvu lakini mara kwa mara bila neema. Kwa hiyo neno linakuwa ***"Andiko linaloua"* 2 Kor 3:6.** Kuna wahuduma wengi na waamini ambao wanaenda wakieneza 'neno' kulingana na ufahamu wao na utafsiri. Lakini mazao ya haya yamekuwa migawanyiko na mara kwa mara kujitenga, badala ya mwili uliojaa neema wakifanya kazi pamoja na kuenenda katika ukamilifu.

Agano jipya ni sehemu nne neema na sehemu mbili kweli!

Ni wakati wa **kukua katika neema** na maarifa (**kweli)** ya Bwana na Mwokozi Yesu Kristo! Ni wakati wa kupokea **neema** ambayo inawezesha utume (kuhubiri **kweli)** kuenenda ambako kutaleta utiifu wa imani miongoni mwa mataifa yote.

Ni neema inawezesha huduma ya neno (**kweli)** na ni **neema** ambayo inawezesha kuhudumu (kutumikia) mmoja na mwingine katika unyenyekevu, alama ambayo ni utiifu kwa Mungu na mmoja na mwingine, ambayo itajenga uhusiano wenye kumaanisha ambao mwili utajengwa pamoja katika Kristo.

Kupitia NEEMA → (ili MUNGU) ← kupitia KWELI
Ikiwezesha Uhusiano → (apate) ← kuleta ufunuo
Kwa kuhudumiana mmoja na mwingine → (atukuzwe) ← kwa kunena neno

Maagano haya ya neema na kweli ambayo imefunuliwa kupitia Kristo Yesu inafanya kazi tu tunapokuwa na mchanganyiko unaofaa: neema sehemu nne na kweki sehemu mbili. Hebu ombi letu liwe:

Mungu tuonyeshe jinsi ya kukaribia enzi ya neema ili tuweze
kukua katika neema ili huduma yetu ya neno iujenge
mwili wako na sio vikundi vyetu ama dini.

FARIJIANENI KWA MANENO HAYA

Kubadilishwa kwa watakatifu

Moja wapo wa siri za neno la Mungu ni 'kubadilishwa kwa watakatifu' kutoka kwa miili ya ulimwengu mpaka kwa miili ya utukufu na tunafahamu haya yatatendeka wakati "***Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni"* 1 The 4:16.** Paulo anaiita siri, ***"Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika"* 1Kor 15:51-52**. Paulo anaeleza siri hii zaidi, ***"kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakaeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake"* Flp 3:20-21.**

Wale ambao wamekufa

Mtume anatuambia kwamba hataki "***msijue habari zao waliolala mauti* (waliokufa)…*hao waliolala katika Yesu"* 1The 4:13-14.** Paulo anaongea juu ya wakristo waliokufa au kama tusemavyo 'wameenda kuwa na Yesu', kwa maana hapo ndipo walipo. Watu mara kwa mara wanauliza 'unaenda wapi unapokufa kama wewe ni mwamini?' Paulo anaseama ***"Wakati tuwapo hapa katika mwili, tunakaa mbali na Bwana"* 2 Kor 5:6.** Kwa maana Yesu alikufa na akafufuka tena, ambao wamekufa katika imani wamekwenda kuwa na Bwana. "***Lakini tuna moyo mkuu; nasi tunaona ni afadhali kutokuwamo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana"* 2 Kor 5:8.**

Watafufuliwa

Kufufuka kwa Yesu kutoka wafu ndio jambo la muhimu sana la imani kwetu na kwa sababu Kristo amefufuka katika wafu tunatazamia kufufuliwa kwa wafu. "***Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala"* 1 Kor 15:12-20.**

Kwa Neno la Bwana

Katika **1 The 4:15** Paulo anasisitiza, ***"Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana".*** Paulo anataka tujue siri ambayo ako tayari kuifunua ni ufunuo alioletewa na '**Neno la Bwana'.** Jambo litatendeka katika ***"kuja kwa Bwana";*** na itawahusisha wafu katika Kristo na waamini duniani ambao wanatazamia kuja kwake. Kutakuwa na kizazi cha waamini (watakatifu) ambao watakao kuwa hai wakati Bwana Yesu atakuja. Lakini kuja kwake kunahusisha "***Mungu atawaleta pamoja naye waliolala katika Yesu"* aya 14.** Mungu atawaleta pamoja na Yesu wakristo wote waliokufa na wamekuwa naye katika himaya ya mbibguni.

Kufufuka kwa mwili

Wafu katika Kristo hawajalala kaburini kana wengine wanavyofundisha kimakosa; tayari wako na Kristo mbinguni na miili yao ya roho. Tunao mwili wa asiri na mwili wa kiroho na nafsi zetu zinaunganishwa na (au sehemu ya) mwili wetu wa roho. Wakati mtu anakufa ni mwili wake wa asiri unakufa. Nafsi ya mtu ambayo inaunganishwa na sehemu ya kiroho imeumbwa kwa umilele. Paulo anaweka wazi katika aya hizi katika **1 Wathesalonike 4** na **1 Wakorintho 15** kwamba wafu katika Kristo wako na Bwana sasa na kwamba kuna kufufuliwa kwa miili yao siku sijazo.

Yesu atashuka kutoka mbinguni

"*Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni"* 1Wathesalonike 4:16; Yesu anakuja kutoka mbinguni. Yesu amepokelewa mbinguni ***"hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote"* Mdo 3:20- 21** lakini katika kuja kwake atashuka hapa duniani "***akija juu ya mawingu ya mbinguni"* (Mt 27:64, Mk 14:62, Mt 24:30).**

Malaika waliwaambia wanafunzi ***"Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni"* Mdo 1:11.** ***"akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao"* aya 9.**

Sauti

Kushuka kwa Bwana kutoka mbinguni kutatangazwa ***"na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu"* 1 Wathesalonike 4:16.** Katika agano la kale watu wa Mungu waliambiwa ***"Wampigie Mungu kelele kwa sauti ya shangwe"* Zaburi 47:1.** Sauti ilikuwa ni kielezo chenye nguvu cha sifa. Katika kuchukua Yeriko sauti ya parapanda na ***"Sauti kuu"*** zilikua za muhimu katika kuuangusha ukuta (**Yoshua 6:20).** ***"Mungu amepaa kwa kelele za shangwe, BWANA kwa sauti ya baragumu"* Zaburi 47:5.** Wengine wanasema kwamba huu ni mtazamo wa kinabii wa kupaa kwa Yesu katika **Mdo 1:9-11**. Hakika ni mtazamo wa sauti ya Mungu! Mtu anaweza kushangaa tu kwa nguvu na mamlaka ya sauti hiyo.

Sauti ya malaika mkuu

"Sauti ya malaika mkuu" ni ukweli usiojulikana. Katika Biblia ni mikaeli anayetajwa kama malaika mkuu (**Yuda 9**). Mikaeli pia anatajwa kama ***"mkuu" (*Danieli 10:21**) na ***"jemadari mkuu"*** (**Danieli 12:1**). Kwa hivyo sauti ya malaika mkuu inaweza kueleweka kama sauti ya Mikaeli!

Mikaeli kama malaika mkuu ana mamlaka makuu na nguvu. Kuna aya nyini za malaika katika **Ufunuo** kwa mfano, ***"na Yule malaika niliemwona akisimama juu ya bahari na juu ya nchi..."*** (**10:5**)**;** ***"kisha nikaona malaika mmoja amesimama katika jua; akalia kwa sauti kuu"*** (**19:17**)**.** Hatujui kwa ujuzi wetu wa sasa viwango na ukuu wa malaika wakuu wa Mungu lakini tunaweza anza kufikiria **sauti ya malaika mkuu.**

Parapanda ya Mungu

"Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, (Kiyunani '*atomos'* ambapo tunapata jina atom wakati huu ni kama sekude ya atom), ***kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho, maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika"* 1 Kor 15:51-52.**

Kuna mahali pengine pa kuangalia habari ya 'parapanda' katika **Mt 24:31** ambayo inatuambia ***"Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake kutoka pepo nne".***

Baragumu */ shophar*

Miaka ya hapa punde tarubeta ya biblia (inatamkwa *shoh-fahr* baragumu iliyotengenezwa kutoka kwa pembe ya mnyama iliyojipinda) imepatianwa kanisani kufanya kanisa ijue habari za baragumu. Baragumu ililia katika mlima wa Sinai ikitangaza kushuka kwa Bwana (**Kutoka 19:16, 19-20**). Hii ni ya muhimu kwa kuwa baragumu itasikika tena Bwana atakaposhuka toka mbiguni.

Baragumu pia ilipigwa katika **Yoshua 6:1-20** kama silaha yenye umuhimu katika kuangusha kuta za Yeriko. Baragumu ilitumika kutahadharisha (**Ezekiel 33:2-9**). Baragumu ilitangaza siku ya upatanisho, mwaka wa kukubalika (**Law 25:9**) na kurejeshwa kwa saduku (**2 Samweli 6:15**).

Kwa dakika

Maandiko yanasema kushuka kwa Yesu kutatangazwa kutoka mbinguni kwa **Sauti, sauti na baragumu.** Hatuwezi kufikiri maajabu ya 'dakika kidogo' wakati Bwana atashuka kutoka mbinguni, akiambatana na roho za wote waliokufa katika Kristo na pengine na malaika wengi. Henoko alitabiri ***"Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu"*** **Yuda 14**

Kumlaki Bwana hewani

"*Nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza"* 1 The 4:16. ***"Roho za wenye haki waliokamilika"*** **Ebr 12:23** ndio watakatifu walio mbinguni, lakini wanakuja duniani na Yesu kuupokea mwili wao wenye utukufu. Katika njia zizizoelezeka miili yao itafufuliwa kutoka ulimwenguni!

"Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, (watakatifu walio ulimwenguni wakati wa kuja kwa Bwana) ***tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili tumlaki Bwana hewani"*** **Aya 17.** Huu ndio wakati ambapo ***"Uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa"*** **1Kor 15:53**

Yesu anakuja kutoka mbinguni mara moja

Kuna kuja kumoja tu kwa Bwana Yesu Kristo kutoka mbinguni hadi ulimwenguni: **atashuka!** Yesu atakuja kwa himaya ya ulimwengu. Tutamlaki ***"hewani":***

- Tutakaponyakuliwa kumlaki, itakuwa ni hewani
- Mahali tutakaponyakuliwa kumlaki, itakuwa ni hewani.

Mawinguni

Hakika tutanyakuliwa ***"Mawinguni".*** Tumeonyesha kuja kwake mawinguni hapa juu na sasa tunataka kutaja **Waebrania 12:1** ambayo inazungumzia watu wa imani kutoka agano la kale ambao wako mbinguni na Yesu kama ***"wingu kubwa la mashahidi".*** Pengine 'mawingu yenye nguvu' ambao Yesu atakuja juu yake kama ilivyotabiliwa katika **Danieli** na Yesu mwenyewe katika injili hakika ni ***"maelfu maelfu ya watakatifu wake".*** Hakuna uhakika katika **1The 4** na maandiko mengine ambayo tumepatiana, kwamba Yesu atakuja mara mbili, kwanza kulipeleka kanisa mahali, na kisha kuja ulimwenguni kuwahukumu wasiomjua Mungu.

Na tutakua pamoja na Bwana milele

Mtume kisha anasema "***Na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele"* 1 The 4:17.** Ufahamu wowote tulionao wa kuja kwa Bwana, jambo la muhimu ni kuwa tayari kumlaki Bwana hewani ili tuwe naye milele.

Mateso na adha

Katika **2 Wathesalonike 1na2** kuna mazungumzo mengi na maelezo kuhusu kuja kwa Bwana. Katika **1:4-5** kanisa linapitia mateso na adha na neno la Mungu linaahidi kwamba watesi wa kanisa watalipwa na Mungu "***kwa mateso"* aya 6.** Mungu atapatia ***"ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na***

malaika wa uwezo wake"* aya 7.** Jambo la kawaida la kusoma maandiko haya ni ya kuwa kanisa litapitia mateso kama halijafanya hivyo (kama Uchina ambapo kanisa limepitia mateso mengi kwa miaka 55 iliopita) na litakombolewa kwa mateso hayo "wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni".*** Atafunuliwa kutoka mbinguni na malaika wa uweza wake ***"katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu"* aya 8.**

Atakuja kwa hukumu

Kuja kwa Bwana kwanza kutadhihirishwa kwa watakatifu ulimwenguni. Wafu katika Kristo watakuja na Yesu kutoka mbinguni, wakitumwa na Mungu, na miili yao ya utukufu itafufuliwa kutoka dunia na tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu kumlaki Bwana hewani.

Kisha wengi wanafundisha kwamba kanisa la watakatifu ambao wako hai katika kuja kwake na wafu katika Kristo watakaokuja naye watapelekwa maeneo ya mbinguni kwa kipindi fulani. Hata hivyo mafundisho kama hayo hayana msingi katika maandiko kama yalivyo nakiliwa katika **Wathesalonike 1na2.**

Katika nyakati za mateso na adha

2 Wathesalonike 1 inaonyesha wazi kanisa wakati wa mateso na adha ambayo sio mengi wakati wa kuja kwa Bwana ambaye anakuja kwa hukumu kwa wale ambao hawamjui Mungu na wale ambao hawaamini injili.

"Watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake".

Kuna watu ngazi mbili ambao watahukumiwa:

- '**Wale wasiomjua Mungu'.** Hawa ni wale ambao wanaabudu sanamu- miungu ilioumbwa na mikono ya wanadamu au wale wasioabudu kitu lakini matakwa yao wenyewe na mipango,
- '**wale ambao hawaitii injili** ya Bwana wetu Yesu Kristo': hawa ni wale ambao wamesikia injili lakini wamekataa kuamini.

Neno 'kutii' linamaanisha *kusikiza, kushughulikia.* Neno la injili linatakiwa kusikizwa na kushughulikiwa: hiyo ndio utiifu. Yesu ameamuru kanisa ***"kuhubiri injili kwa kila kiumbe"* Mariko 16:15.** Kisha anasema wale ambao hawaamini injili watahukumiwa **aya 16**.

Na watakatifu

Mapema tulitaja unabii wa Henoko katika **Yuda 14** akizungumzia waliokufa ndani ya Kristo wakiandama na Yesu kutoka mbinguni. Hata hivyo wakati tunatazama unabii huu katika mazingara haya, Bwana yuaja na watakatifu wake "***ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu wameyanena juu yake"* Yuda 15.**

Hii inamaanisha kwamba watakatifu ambao wanakuja na Yesu kuleta hukumu wanahusisha wafu ndani ya Kristo ambao wameupokea mwili wao wa ufufuo na watakatifu waliohai ulimwenguni na wainuke kumlaki Bwana hewani wakiipokea miili yao ya utukufu. Yesu Kristo anakuja kwa hukumu na watakatifu wake wa kweli, waamini, waliotakaswa ambao wametukuzwa ndani yake na kuunganishwa naye hewani, waja naye kutawala na kutamalaki duniani kwa miaka elfu moja.

Kutukuzwa katika watakatifu wake

Ni lini wasioamini na wasiotii watahukumiwa? ***"Yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, kustaajabiwa katika wote walio sadiki katika siku ile"*** **2 Wathesalonike 1:10.** Kuja kwa Bwana inaleta mambo mawili yenye umuhimu: kutukuzwa kwa watakatifu na hukumu ya waovu. Kuja kwake na hukumu ni siku moja na atakapotukuzwa katika watakatifu wake. Atatukuzwa katika watakatifu wake watakapoupokea mwili wao wa utukufu na hayo yatatendeka wakati ***"Atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo"*** (**1 Yn 3:2**)**;** wakati ***"tutanyakuliwa Kristo nao katika mawingu ili tumlaki Bwana hewani"*** (**1 The 4:17**)**.**

2 The 1:10 inapendekeza kwamba kuna vikundi viwili watakaompokea Bwana ulimwenguni:

- **Watakatifu ambao Bwana atatukuzwa ndani yao,**
- ***"Wale wote wanaoamini"* - waumini.**

Pengine kutakuwa na umati mkubwa duniani ambao kwa furaha watamkubali Mfalme akirudi ambao hawajahesabiwa Kristo na watakatifu ambao wamejiandaa kwa kuja na wamedhawabiwa kwa kuwa ***"na Bwana milele"*** kwa hali ya kutukuzwa.

Kuna mafundisho mengi Krist juu ya kuja kwa Bwana. Hatuna mda wala ufahamu tosha wa **2 Wathesalonike 2** ambayo inaongea juu ya kufunuliwa kwa yule mtu wakuasi ***"mwana wa uharibifu",*** kufundisha juu ya aya hizo sasa.

Lakini ambacho tunaweza kusema ni ***"Hapo ndipo atakapofunuliwa yule asi, ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake"*** **2 Wathesalonike 2:8**. Tena **ni kuja kwa Bwana kutakakokabiliana na yule asi.**

Kama vile tumeona katika fundisho hili **kuna kuja mara moja tu kwa Bwana** na ni wakati wa kanisa kuwa tayari kwa kuja kwake. Hii inahusisha kuwa imara na kuja katika kufahamu kwa undani wa neema yake kutuwezesha kusimama katika nyakati za Kristo mateso, tukilitangaza neno la Bwana na Ubwana wa Yesu Kristo.

UFALME WA MUNGU, KUJA KWA BWANA, UJUMBE WA UWANA

Katika safari za ng'ambo mapema 2007 nilikuwa nikihubiri injili ya ufalme na kufundisha neno la Mungu kwa siku kumi na nne na kisha nikarudi nyumbani.

Ujumbe mkuu ulikuwa:

- **Ufalme wa Mungu –** kuingia ndani yake na kupokea ufalme kama urithi ulioahidiwa;
- **Kuja kwa Bwana –** kuwa umejiandaa na kuwa tayari kwa kuja kama ilivyo kinyume cha kunyakuliwa kwa ghafla, na hiyo inamaanisha kukamilishwa;
- **Ujumbe wa kufanyika wana -** kuja katika ukomavu, kupokea neema ya kutembea katika ukomavu, ambayo ndiyo njia ya kukamilishwa.

Majuma hayo mawili yalipopita jambo moja lilikuwa wazi kwangu! Hakuna shaka kwamba neno la mwaka wa 2007 lilikuwa '**ni wakati wa kupokea ufalme' Luka 12:32.** Hata hivyo pasipo neema ya uwana ikifanya kazi ndani ya maisha yetu katika kristo hatutaandalika kuupokea ufalme wala kuwa tayari kwa kuja kwa Bwana, utimilifu wa ufalme ulimwenguni.

Urithi ni ufalme!

'Siraha za vita vyetu sii za Mwili' - 2 Wakorintho 10:4-6

Vita vyetu vya kibinafsi sio kingine ila mtu aking'ang'ana ndani ya mwili, akitafuta kuzikumbatia ahadi za Mungu kwa kukiri kwa nguvu na mengineyo. Mambo matatu muhimu ambayo Mungu ametoa ili kutembea katika ushindi: **toba, unyenyekevu na utakatifu.**

Toba

Hii ni kifunguo cha kuwa na mabadiriko ya mawazo yetu yakigeuzwa, ikielekeza katika kufanywa upya kwa mawazo ambayo ndiyo njia ya kugeuzwa, tukija kikamilifu kwenye mapenzi ya Mungu (**Warumi 12:2**). Toba ni njia ya kuingia kwa ufalme. Yesu alisema ***"Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini injili"*** **Mariko 1:15.** Toba ndio msingi wa kwanza katika Kristo: ***"Kuzitubia kazi zisizo na uhai"*** (**Ebr 6:1**).

Vita vyetu vingi vimekuwa ni kazi zisizo na uhai. Toba ya kweli hakika inaelekeza ***"kuwa na nia ya Kristo"*** (**1Kor 2:16**)**.** Kama nia yetu ni ya kuwa unataka kubandilisha mawazo yako [Neno la Kiyunani la 'toba' *Metanoia* na inamaanisha 'kugeuza mawazo'] kisha Bwana anaweza kutuleta katika ufunuo kamili wa hekima ya Mungu ya dani.

Unyenyekevu

Hii ndio funguo ya neema, ***"kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema"*** **(1 Pet.5:5b).** Ni tunapojinyenyekesha ambapo Mungu hutuinua akionyesha utukufu wake kupitia sisi (**1Pet.5:6**). Funguo za kutembea katika utukufu wake ni neema yake na ni wakati tu tunapoifikia neema kamili ambapo tunamwagiwa tunapopokea roho wa kufanywa wana ambapo tutaweza kujiandaa kwa kuja kwake.

Neema ilikuja kwa njia ya Yesu Kristo: "***Kwa kuwa katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema"*** (**Yohana 1:16 NASB**)**.** Mitume walioziandika nyaraka wakati wote wanatuhudumia neema kwa mwanzo wa nyaraka zao na Paulo anatamatisha nyaraka zake na kutuhudumia neema. Paulo ako wazi ya kuwa ufunuo wake wa siri ilimjia kupitia majira ya neema spesheli (**Efe 3:2-3&8**), na hivyo hivyo ili sisi tuijue siri tunahitaji majira spesheli ya

neema. Hii ni neema ambayo inaachiliwa wakati tunapokea roho wa kufanywa wana, ikituleta katika uhusiano wenye ukomavu na Bwana kama Baba na kuweza kupokea hekima ya ndani ya Mungu **(1 Wakorintho 2:6-8**).

Utakatifu

Hii inamaanisha kutengwa na tunatakiwa kuwa tumetengwa kwake kikamilifu "***tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu"*** **Ebr 12:2.** Ilikuwa ni BWANA mwenyewe ambaye ***"aliitenga kabila ya Lawi ili walichukue lile saduku la agano la BWANA, wasimame mbele ya BWANA kwa kumtumikia, na kuwabariki watu kwa njina lake"*** **Kum 10:8.**

Kama tukijipatiana kwa Bwana katika maisha yetu yote tutapata kwamba atapatiana kiingilio kwetu ***"kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, mwokozi wetu Yesu Kristo"*** **2 Petro 1:11.** Uhakika wa ajabu ni kuwa Mungu anafanya kazi ndani yetu. Sio kulingana na kazi zetu au kazi za sheria, lakini ni ***"kwa imani ilio katika Kristo",*** ni ***"haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani"*** **Wafilipi 3:9.** Mungu ni mtakatifu na tunapomjia atatufanya kuwa watakatifu. Dhawabu ya kuwa tumetengwa kwa Mungu ni kuwa urithi unapeanwa na Mungu kwetu. Hii ilikuwa hivyo kwa Walawi (**Kum 10:9**) na ni hivyo kwetu leo

'Wito wa pamoja wa Uwana'

Mungu analiita kanisa kwa pamoja kuja katika ukomavu, kupokea roho wa kufanyika wana, kufanyika huyu mwana aliyenenwa katika **ufunuo 21:7 "*Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu".***

Mpaka hivi punde tumekuwa tukiwaita watu kibinafsi katika uwana na ndio kila ujuzi katika Kristo unapatianwa kwa watu binafsi, lakini mabandiliko ambayo yamekuja katika ufahamu wetu ni kwamba **Mungu analiita kanisa lake kwa pamoja katika uwana.**

Wakati wa uwana ni ***"uliokwisha kuamriwa na Baba" Gal 4:2.*** Sio wakati ambapo tunajidhania kwamba tumekomaa vya kutosha kwa maana sio kulingana na kazi zetu bali kulingana na neema.

Hata kama vile tuliokolewa kwa neema kupitia imani, hivyo ndivyo ilivyo, kwamba sasa tunaweza kuingia katika uwana kupitia neema kwa njia ya imani na imani hiyo huja kwa kusikia neno (**Rum 10:17**). Mpaka hivi punde kanisa halijasikia neno kuhusu 'kuwekwa mahali ambapo panakufaa' ama sawa 'uwana'. Kama vile neno limehubiriwa, imani inakuja. Imani inapokuja milango ya neema inafunguka na tunawezeshwa na neema kutembea katika yale tumeamini.

Kuurithi ufalme

Lengo la Mungu kwa 'mwana' katika umoja kuja ulimwenguni: hawa ndio watu ambao maisha yao ***"yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu, Kristo atakapofunuliwa aliye uhai wetu ndipo nanyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu"*** **Kol 3:3-4.** Hawa ni wale ambao wamesikia wito wa kuja katika ukomavu; hawa ni wale ambao wamepokea ufalme wa Mungu kama urithi ambao tunatembea hapa ulimwenguni. Ufalme huu ni ***"haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu"*** **Rum 14:17.** Ufalme huu hauji kwa kutizama au kuzingatia sheria za ndini. Ufalme huu kwanza unaingiwa kupitia kuzaliwa upya. ***"Kilichozaliwa na roho ni Roho"*** **Yohana 3:6.**

Ufalme ni sasa na ufalme unastahili urithiwe.

Mfano wa ngano na magugu

Hebu tutizame kwa kifupi mfano wa magugu katika **Mathayo 13:24-30**, na kama ilivyoelezwa na Yesu katika aya ya **36-43**. Huu mfano unatupatia ufahamu wa ndani wa maana ya kurithi ufalme na vile inahusiana na kuja kwa Bwana. Yesu anatuambia wazi mpanzi wa **mbegu njema ni mwana wa adamu** na anazipanda mbegu njema ulimwenguni, **konde. "*Zile mbegu njema ni wana wa ufalme".*** Wana wa ufalme lazima wawe watakatifu wakitembea katika Roho wa kufanyika wana.

Hukumu itawatoa waasi ulimwenguni

"*Magugu ni wana wa yule mwovu"* ambao wako ulimwenguni na ni wana wa ibilisi, "***na yule adui aliyewapanda ni ibilisi".*** Kisha Yesu anatuambia "***mavuno ni mwisho wa dunia; na wale wavunao ni malaika".***

Malaika ni wakina nani? Neno la kiyunani *angelos* SC#32 kutoka kwa *angello* 'kupeleka ujumbe, kuleta habari, inamaanisha 'mjumbe', na kijumla inatafsiriwa 'malaika'. Katika Mfalme Yakobo Agano jipya neno hili limetafsiriwa malaika mara 179 na 'mjumbe' mara 7. Ni maamuzi ya watafsiri ni tafsiri gani inayofaa katika mazingira ya kifungu. Kwa habari za Yesu juu ya mfano inaweza kufaa sana kutafsiri *angelos* kama 'mjumbe' kwa maana Mungu hajaweka injili kwa malaika bali kwa watu. Ni mitume ambao Yesu alifundisha na akawatuma kwenda kuvuna mioyo na kuwaleta watu katika ufalme, sio malaika.

Katika mwisho wa dunia magugu [ambao wanakosa na kutenda maasi] "***watakusanywa nje ya ufalme wake"*** na malaika/wajube. Wataondolea ulimwenguni na "***kutupwa katika tanuru ya moto"*** **aya 42.**

Tafadhali elewa kwamba ni 'wale waovu' ambao watakaoondolewa au kuhukumiwa. Hii inadhibitishwa wakati Yesu anapolinganisha siku ya kuja kwake na siku za Nuhu, "***gharika ikaja ikawachukua wote"*** **Mt 24:39.** Waasi walichukuliwa na gharika na mafuliko ambayo ilikuwa ni hukumu ya maji.

Kisha Yesu akaongea "***watu wawili watakuweko kondeni, mmoja atwaliwa mmja aachwa. Wanawake wawili watakuwa wakisaga, mmoja atatwaliwa mmoja ataachwa"*** **Mt 24:40-41.** Wengi wametwambia yule aliyetwaliwa hapa ni Yule mwenye haki aliyepelekwa mbinguni. Hata hivyo Yesu alisema '***itakuwa kama siku za Nuhu'*** na ni wazi ni waasi waliotwaliwa na gharika na wenye haki wakaachwa, hivyo ni **wakaokolewa na maji na wakahifadhiwa ulimwenguni.**

Ufalme unarithiwa hapa ulimwenguni

Mwisho wa maelezo ya mfano wa Yesu wa ngano na magugu inatuonyesha kwamba ufalme utarithiwa hapa ulimwenguni. ***"Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao"*** **Mt 13:43.** Hawa ndio watakatifu, ***Wana wa ufalme,*** ambao wanarithi ufalme wa Mungu ulimwenguni! ***Watang'aa kama jua!***

Wakati Yesu alibadilishwa, ***"Uso wake ukang'aa kama jua"*** **Mt 17:2.** Mabadiliko yalifanyika hapa ulimwenguni Yesu akiwa katika mwili wa mwanadamu. Kubadilishwa kwa Yesu ni Mfano wa utimilifu kwamba tumewekewa hatima kurithi tunapokuja katika utimilifu wa kufanyika kuwa wana, ambayo ni ***"ukombozi wa mwili wetu"*** **Rum 8:23.**

Ni wana wa ufalme ambao watarithi ufalme wakati wa mwisho. Ufalme wa Mungu unaimarishwa hapa duniani, tayari kwa kurudi kwa Mfalme.

Ameketishwa

- *"Neno la BWANA kwa Bwana wangu, 'uketi mkono wangu wa kuume, hata niwafanyapo adui zako kuwa chini ya miguu yako'"* **Zaburi 110:1,**
- *"Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake"* **1Kor 15:25.**

Kwa kutamatisha twapaswa kupokea Roho wa uwana kuhitimu katika kupokea urithi ambao ni ufalme wa Mungu na tunapotembea katika urithi huu wa ajabu tutakuwa tumejiandaa vyema na kuwa tayari kwa kuja kwa Mfalme Yesu.

UFUNUO WA KIUTUME

Kuokoka, kubatizwa na karama ya roho

Ninafurahia katika Bwana na kulishukuru jina lake kwa neema ya ajabu ambayo ametujulisha kupitia ufunuo wa kitume ambayo amekuwa akifunulia kanisa lake. **Nimeokolewa, nimebatizwa kwa maji na kujazwa na Roho kutoka kati ya mwaka wa 1974. Wokovu kwangu ulikuwa ni jambo kubwa la mabadiliko ya maisha.** Kuanzia siku niliyookoka, nilijua nilikuwa; nilijua nimekutana na Yesu Kristo; nilijua nimezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu.

Ilikuwa ni ajabu! Ilikuwa ni Bwana aliyeniongoza kwa ubatizo wa maji kwa kuwa hakukuwa na watu waliokuwa wakiongea juu ya ubatizo wa maji katika kikundi cha watu wa kiroho ambao niliokoka ndani yake (**Mariko 16:16**). Ilikuwa ni Yesu Kristo aliye nijia majuma machache baadaye na akaachilia Roho wake ndani yangu kuthihirishwa kwa lugha ya mbinguni akiniwezesha kuomba ndani ya Roho kwa Mungu tangu wakati huo, nikijijenga (**1Kor 14:2,4**).

Uwanafunzi, utumishi na uongozi

Kuanzia dakika niliyookoka nilitamani kuwa mhubiri na kwa kujitakia nikaingia katika kila fulsa **kufundishwa neno la Mungu.** Nilitafuka watu ambao wangeshiriki neno nami. Nilitamani kwenda katita chuo cha Biblia lakini hakukua na milango iliofunguka siku hizo.

Nilipokua katika Kristo nilichukua kila nafasi **kutumika katika kanisa la mahali pamoja,** mwanzo nikifanya kazi zote za mikono katika jengo na kusaidia katika kazi za shemazi. Kwa haraka sana nililetwa kwa uongozi na nikaanza **kuongoza ushirika nyumbani kwetu.** Wakati huo ulikuwa na changa moto sana kwa maana nilikuwa sijaandaliwa. Tulikuwa na wachungaji wachanga na bila akina baba, bila mitume, bila mtu wa kutuelekeza na kutufundisha juu ya huduma.

Kutiwa nguvu na Roho mtakatifu

Mwisho wa mwaka wa 1994, nilitumika katika uongozi wa dini moja iliofaulu katika mji wetu na wachache wetu walihusika katika huduma wakawa **wakichangwa moto sana na ushuhuda wa kanisa katika kitabu cha Matendo**. Hata kama tulikuwa 'Wakiroho' katika huduma yetu, tulijua kwamba tuna sehemu kidogo sana ya "***nguvu"*** za Roho Mtakatifu ambaye Yesu aliahidi katika **Mdo1:8**. Tulianza kumtafuta Mungu kwa bidii na mnamo Januari 1995, niliita mikuta ambapo tuliabudu na kumgonjea Bwana.

Roho Mtakatifu akaja juu yetu kwa njia kuu na wengi wetu wakawa na ujuzi wa maisha yao kubadilishwa. Yawezekana kuwa kweli kwamba daadhi yetu tulikuwa tunanena kwa lugha na kuhudumu katika karama zingine za Roho kwa miaka mingi hapo awali lakini katika kipindi hiki **tulipokea ujazo wa nguvu na tukaanza kutembea ndani ya Roho kwa njia inayoonekana.** Pamoja na wengine, mara kwa mara sikulala usiku lakini **ningechukuliwa ndani ya Roho nikipokea ufunuo, niliishi katika himaya iliyokuwa ya kiroho sana kuliko ya ulimwengu.** Ningeenda kazini siku iliyofuata nikiwa mchangamfu na mwenye nguvu.

Kama matokeo ya ujuzi huu wa ajabu tukaanza kufanya mikutano mingi kwa kanisa hilo na kisha tukaanza kutembea katika maeneo mengi Aaustralia, tukifanya mikutano ya uvivio **tukishuhudia wokovu, uponyaji, ujazo wa Roho na ishara na maajabu za kushangaza.**

Kipindi hiki kiliendelea kwa miaka minne ikihusisha mwaka wa kwanza wa huduma ya uvivio ya Australia [RMA ilianza huduma katika Januari 1998]

Neema ya mtume wa kweli

Katika mwezi wa nane 2001, nilipata fulsa ya kukutana na mtume mwingine na akaja SHILOH [kituo chetu Toowoomba] kutufundisha. Nilijua kwamba nilikuwa nimeitwa niwe mtume na nilikuwa nimeanza kuhudumu katika ngazi hiyo. [Bwana Yesu alikuwa amenitokea mnamo Januari 1998, akinituma kwa huduma ya mtume].

Mtume aliyetujia **aliongea juu ya neema kwa njia ya kustaabisha na ya kusikika; aliachilia neema ya Mungu kwetu**. Sote tulijua kwamba tumeokolewa kwa neema; tulijua kwamba karama za kiroho ni vipawa vya Roho katika kazi ['charis' ni neno la Kiyunani la neema] lakini sasa tulikuwa tukihisi neema kwa njia mpya na pana. Tulitambua kwamba **moja wapo wa maelezo ya mtume ni neema ambayo mtume anatembea ndani yake, anahudumu ndani yake, na anaweza kugawa.**

Ni ya muhimu kumpokea mtume kama mtume. Yesu alisema katika kuwatuma mitume wa kwanza ***"Awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenituma"*** **Mt 10:40.** Tulijua kumpokea ndugu aliyekuja kama mtume na sote tukapokea neema zaidi kuliko hapo mwanzo kwa kuwa tulimpokea mtume wa Yesu Kristo.

Ufunuo wa kitume

Msemo huu, ufunuo wa kitume inakamata kwa umuhimu ambacho Mungu amepatiana kwa kanisa la siku za mwisho. Ni ufunuo wa kitume ambao unatuleta kwa **mabadiliko makuu, maisha ya mabadiliko na ujuzi** ambayo yanaendelea kufunuka siku baada ya nyingine na inaweza kuhudumiwa wengine kwa upana na umbali. Kama matokeo ya kupokea neema ya Mungu kuamini ufunuo wa kitume, ambayo ni huduma ya neno iliyojaa neema na upako, tumetiwa nguvu kuachilia hiyo neema kwa wengi na kushuhudia wakipokea mababiliko makuu, maisha ya mabadiliko.

Kuwekwa kama wana

Kila siku tunashukuru Mungu kwa neema yake. Twajua kutoka kwa neno kwamba hii ni '**kutembea katika uwana',** tukiisha kupokea hatima ***"ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo sawa sawa na uradhi wa mapenzi yake"*** **Efe 1:5.** Ni kwa mwisho wa nyakati ambapo Mungu anawaita kanisa wapate kutembea katika ukomavu. Wana wa Mungu ni warithi na warithi pamoja na Kristo (**Rum 8:17**) ***"Lakini wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote; bali yu chini ya mawakili na watunzaji, hata wakati ulipokwisha kuamuriwa na baba"*** **Wagalatia 4:1-2.**

Kanisa kwa kizazi hiki halijakuwa katika ukomavu. Twaweza kuwa tumehitimu kutoka kwa watoto kufanyika watumishi, hivyo ni, wahuduma, lakini hatujatembea katika urithi wetu kama wana. Lakini sasa Mungu anarejesha akina baba na ni akina baba [mitume] ambao Mungu anainua ambao kwa wakati unaofaa wanaachilia watoto ambao wamekuwa watumishi katika uwana kwa Mungu.

Ninashuhudia kwamba Mungu amenileta katika ufunuo wa neema yake na amenijulisha **roho wa kufanywa wana,** akanifunulia **uhakika wa kufanyika kuwa mwana wa Mungu. (Yn 1:12, Ebr 2:10, Rum 8;19).** Neema hii inaniwezesha na wandugu tulionao katika kikundi chetu

cha kiutume cha SHILOH na wandugu wengi kote katika Mataifa kutembea katika ukomavu. Sasa twajua kwamba neno la Mungu litatimizwa.

Twafahamu kwamba Yesu ***"Atajiletea kanisa tukufu"*** **Efe 5:27.** Twashuhudia kwamba huduma tano katika **Efe 4:11-13** zinainuliwa kufanya ***"Kazi ya huduma, hata mwili wa Kristo ujengwe hata na sisi sote tutakapofikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu…hata kuwa mtu mkamilifu".***

Kuongozwa na Roho

Matokeo ya neema hii kubwa ikifanya kazi katika maisha yetu inaonekana katika kutembea ndani ya Roho na tunda la Roho likidhihirika katika maisha yetu. Zaidi ya yote, wahuduma wengi ambao wamepokea neena na ufunuo wa uwana wanatangaza mabadiliko yanayoonekana katika huduma zao. Wengi wametangaza kuachiliwa kukubwa kwa njia kubwa kwa nguvu za Roho Mtakatifu; wengine wamehisi kuongozwa na Roho kwa njia ya nguvu (**Rum 8:14)**, kuingia kwa milango kuhudumu hata kwa wafalme na mabalozi na kutambuliwa na kopokelewa na viongozi wa selekari.

Wana wanafanyika wakina baba

Jambo la kushangaza kuhusu ufunuo wa kitume na huduma hii ya neema na upako ambalo linawaleta watumishi wa mungu katika kufanyika wana ni kwamba inaweza kuhudumiwa na kila mmoja ambaye amefanyika mwana. Katika siku za mwondoko wa kiroho na hata wakati huu, kila mtakatifu ambaye amebatizwa kwa Roho Mtakatifu anaweza kuhudumu huo ubatizo kwa kuwawekea mikono wengine, vivyo hivyo, kila mwamini anaweza kumwelekeza mtu mwingine kwa Kristo. Ndivyo ilivyo siku hizi kwamba **Mungu anawainua wana ambao wanafanyika akina 'baba', wakiachilia neema na upako kupitia neno** kwa wengine kuja katika uwana.

Ufunuo unaleta mabadiliko

Mimi mwenyewe nilipata neema hii inayoleta mabadiliko ya uwana ikija katika maisha yangu binafsi mnamo 31/10/2002. Kuanzia hapo maisha yangu yamebadilika kabisa. Nimebarikiwa sana kuwa 'nimetoka kwa njangwa' na kuishi katika 'nchi ya urithi'.

Miaka ya jangwa

Miaka ya jangwa kwa wakristo ni miaka ile ambayo maisha sio mepesi licha ya maarifa ya Mungu ambayo tumekuwa nayo na vipawa vya Roho vikifanya kazi katika huduma yetu. Ni wakati wa kutamani kukomaa katika Kristo; kutamani ushindi katika maeneo ya nafsi ambayo inaonekana kubaki vile miaka baada ya miaka.

Kuja nyumbani

Wakati neema ya uwana iliachilikwa ndani ya roho yangu kwanza na Roho Mtakatifu, jambo la kwanza ilikuwa ni kuhisi usalama ndani ya nafsi yangu na jinsi nilivyo elezea ujuzi huu ilikuwa 'Nimefika nyumbani'. Sasa nimefahamu kufanyika mwana ni kuja nyumbani kwa nyumba ya Baba na inaweza kueleweka kwa nguvu katika **Luka 15:18-23** wakati mwana mpotevu alikuja nyumbani.

Urithi

Wakati huyu kijana alipoteza urithi wake wa asiri, baba yake sasa alimpatia urithi wake wa Kiroho. Baba alisema ***"Lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike; mtieni na pete kidoleni na viatu miguuni"*** **aya 22.** Vazi ni vazi ya haki (kuwa katika msimamo unaofaa na Baba kupitia Yesu) na inazungumzia kufunikwa kamili na Yesu ikituwezesha kutembea katika upako na neema yake.

- Vazi linamtabulisha mwana na baba.
- Pete ni mamlaka ya Kristo ambayo ni mamlaka ya baba ikipewa mwana.
- Viatu vina vikwa miguuni, zikimuwezesha mwana kutembea katika urithi.
- Urithi ni ***"Urithi wake"*** **Efe 1:18,** kutembea katika utukufu: ***"Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu"*** **Kol 1:27.**

KWA NINI UWANA?

Ujumbe ni **UWANA,** ambapo tunapokea na kutembea katika neema ya Mungu neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, katika kiwango kilicho kamili. Ndio, kila kitu katika neno la Mungu kinapatikana kwetu ***"Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni Ndiyo; tena kwa hiyo katika yeye ni Amin; Mungu apate kutukuzwa kwa sisi"*** **2 Kor 1:20,** na wakati katika kila hali tunapokuwa sawa na neno katika Kristo, tunaweza kusema **'Ndiyo na Amin'.**

Hata hivyo ujuzi wetu sote tunapokua katika Kristo kwa jumla ni kama ufuatavyo: tunao ujuzi tofauti tofauti ambayo unapata mizizi na kutuimarisha katika upendo wa Kristo, lakini licha 'ya ujuzi ulio inuka sana', lazima tupitie ngazi zinazostahili za kukua ili tuje katika ukomavu. Kuja kwa uwana ni kuja katika kutembea huko katika ukomavu.

Kwa nini uwana?

1. **Kusudi la Mungu ni kuwaleta wana wengi kwa utukufu kupita Yesu Kristo:** ***"Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyoye vimekuwapo, akileta wana wengi waufikie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso"*** **Ebr 2:10.** Sisi tu watoto wa Mungu kwa njia ya kuzaliwa upya, lakini lengo la Mungu ni **'wana'.** Wana ni wale wamekomaa, wakiwa na uwezo wakutembea katika utukufu wake.

2. **Tumezaliwa mara ya pili tufanyike wana wa Mungu: "*Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa…kwa Mungu"* Yn 1:12-13**. Tunapo zaliwa mara ya pili sisi ni watoto, lakini mbegu ya Mungu iko ndani yetu ya kukua hadi ukomavu, tukifanyika wana. Kuna viwango vitatu vya kukua katika kutembea kwetu na Bwana. Yohana anawaandikia ***"Watoto wadogo, vijana na akina baba"*** **1 Yn 2:12-14.** Akina baba ni wale ambao wamekomaa kama wana, sasa wakiwa na uwezo wa kuwa na watoto wa kiroho**.**

3. **Kuachiliwa kwa roho ya uwana ni ishara ya kwamba tuko katika mwisho wa nyakati: "*Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na kuogofya. Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana"* Malaki 4:5-6.** Roho na nguvu za Eliya zinarejeshwa kwa kanisa ili kujitayarisha kwa kuja kwa Bwana. Bwana yuaja kwa "***kanisa lenye utukufu",*** hivyo ni, ***"Wana wengi"*** wakiletwa kwenye utukufu. Kupitia urejesho wa mitume, akina baba wamerejeshwa wenye mioyo ya kweli kwa watoto wa Mungu. Hivyo watoto wanapokea roho wa uwana na kanisa linaanza kuingia katika urithi wake.

4. **"*Tulichaguliwa tangu asili tufananishwe na mfano wa Mwana wake"* Rum 8:29,** na tunapofika umri wa ukomavu ***"tunafanywa wanawe kwa njia ya Yesu Kristo"*** **Efe 1:5.** Ni wakati tunapotembea kama wana wakomavu katika urithi ambao Mungu amehifadhi kwetu ambapo tunaanza kuonyesha utukufu wake. Wengi wameweka kando kurithi utukufu hadi Yeu atakaporudi lakini hakika Mungu ameweka hatima yetu tutembee kwa utukufu unaoongezeka sasa (**2 Kor 3:7-11, 18).**

5. **Watoto hawarithi hata kama *"Ni warithi pamoja na Kristo"* Rum 8:17.** "***Mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa"* Gal 4:1.** Mungu anangojea watoto wakomae ***"ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu"* Gal 4:5,7.** Hii inatendeka tunapo pokea roho wa kufanywa wana ama ***"Roho wa mwanawe mioyoni mwetu"* aya 6.** Hata kama Yesu alikuwa siku zote mwana wa Mungu lakini hakutembea katika roho wa mwana hadi baada ya ubatizo wake, hivyo nasi twapaswa kukua kutoka kwa mtoto mdogo tuwe vijana mpaka mwana aliye komaa, tayari kurithi.

6. **Viumbe vyote vinangojea kufunuliwa kwa wana wa Mungu** kwa maana "***Viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu:* Rum 8:19-21.** Viumbe vyote vinangojea: Huu ni ukweli wa kushangaza! Viumbe vyote vya Mungu viliwekewa laana kwa anguko la mtu wa kwanza. Lakini sasa **viume vyote vinangojea kufunuliwa kwa wana wa Mungu** kukombolewa kutoka kwa laana hiyo.

7. **Hatima ya kufanywa wana ni *"Ukombozi wa mwili wetu"* Rum 8:23,** na hii inathibitishwa katika **Efe 1:13-14 *"na kutiwa muhuri na Roho Yule wa ahadi aliye Mtakatifu. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake".*** Hata sasa Roho huyo ***"aliyemfufua Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa"* Rum 8:11,** lakini hatimaye ***"tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu"* Flp 3:20-21.**

Sisi sote ni warithi wa Mungu katika Kristo. Hiyo inamaanisha kuna urithi wa kupokea ulimwenguni katika siku hizi za utimilifu na urejesho. Kazi ya ukombozi [malipo ya gharama iliyohitajika kumkomboa mwanadamu na viumbe] imemalizwa na Yesu Kristo kupitia mateso Yake, kufa na kufufuka. Amefanya yote! Mungu ***"kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu"* Efe 3:11.**

- Ni wakati wa kupokea urithi wetu wa kiroho!
- Ni wakati wa kuwa salama ndani ya Kristo kama mwana!
- Ni wakati wa kutimiza sehemu aliyo nayo kwetu katika mwili!
- Hatupaswi kuwa watoto tena (**Efe 4:14**).
- Misingi lazima iwe imewekwa sawa ili sisi twenede katika ukomavu (**Ebr 6:1-3**).
- Kutakuwa na uchungu (mateso) kwa sababu ***"ambaye Bwana ampenda, humrudi, naye humpiga kila mwana amkubaliye"*** (**Ebr 12:3-11**).

MTAZAMO WA MAFUNDISHO YA UWANA

Maandiko peke yake

Leo Mungu anarejesha uhakika wa uwana. Kama siku zote za urejesho neno linaendelea katika njia nyingi tofauti likitangaza jambo mpya ambalo Mungu anafanya. Kwa hivyo wengi wanafundisha juu ya uwana, akina baba na wana, moyo wa baba na mengineyo. Twahitaji kubabanua na kuelewa kile maandiko yanafundisha kuhusu uwana. Ni ufunuo unaofunguka na ninatafuta kushiriki baadhi ya mambo ambayo yamekuwa wazi kwa miaka ambayo nimekuwa nikitembea katika uwana tangu 31/10/2002.

Kuna msemo ambao umetokana na urejesho, ambao uliandikwa na Latin, ambao unasema '*maandiko peke yake'.* Msemo huu ukielezwa unasema '*Maandiko ndiyo mamlaka yetu tu ya imani na utendeji'.* Kwa hivyo chochote tunapofundisha lazima kiwe katika mazingira ya maandiko kama yalivyoandikwa. **2Timotheo 3:16** inashuhudia juu ya kuelekezwa kwa kiungu kwa maandiko yote na inatuambia kwamba andiko ***"lafaa kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu mawazo yao, na kwa kuwaongoza na kwa kuwaadibisha katika haki".***

Kama tunahubiri na kufundisha kulingana na maandiko, basi twaweza kuamuriwa na wale ambao wanatusikiza kwa maana wanaweza kuyafikia maandiko; lakini tukishiriki kwa mamlaka kutoka kwa ndoto, maono, neno la kiunabii na mawazo yetu yanayokuwa na ufahamu basi sio kila mtu anaweza kuamua ule uhakika na uaminifu wa mafundisho yetu. Hata kama tuna upako wa nguvu ambao tunaweza kupatiana, hiyo haijathibitisha kwamba neno letu linafaa kimaandiko.

UHAKIKA WA UWANA

Yesu aliwaombea mitume

Ombi la Yesu katika **Yn 17** inatumiwa na wengi kama uweza wa 'umoja wa miondoko ya wachungaji' katika miji, na katika **aya 4-18**, Yesu anaongea wazi juu ya kuwainua na kuwafundisha mitume kwa pahali ambapo ***"alimaliza kazi"*** na alikuwa tayari kuwatuma wale aliwafundisha kama mitume ***"duniani".*** Kisha aya zinazofuata ambazo zinazungumza juu ya umoja wa waamini wote inaleta maana mwisho: ni wakati ambapo mitume wanaondoka wakiisha kufundishwa na kuinuliwa na Bwana, wakifanya wanafunzi na hivyo wakiliinua kanisa, ambapo patakuwa na umoja ambao Bwana wetu aliuombea.

Kikundi cha kitume

Kwa hivyo jukumu la mitume kuja pamoja katika kikundi cha kitume iwe ni mkutano usiopangwa kama ule ambao Paulo alikuwa nao na mitume viongozi kule Yerusalemu ambao anatoa ripoti juu yake katika **Gal 2:1:10**, au kikundi kikubwa katika **Mdo 15** ambacho kilihusisha mitume wote na wazee kutafakali shinda iliokumba makanisa maeneo mengi. Ni katika kikundi cha kitume ambapo ufahamu wa uwana katika maandiko na mafundisho ya biblia mengine yenye umuhimu inaweza kufafanuliwa kwa makubaliano. Hii itawezesha kuhubiri injili kamili kuenea na kutimiza kusudi la Mungu la 'wana wengi katika utukufu'.

Wana wengi katika utukufu

Katika siku zetu Mungu wetu mkuu na mwokozi Yesu Kristo (Yeshua Messiah) anafanya kazi ya ajabu. **Ebr 2:10** inatuambia kwamba ***"ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia***

yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso”. Yesu aliye Masihi tayari amekamilishwa: ***“Naye alipokwisha kukamilishwa”*** **Ebr 5:9.** Sasa Mungu anatimiza lengo lake kuu: ***“Wana wengi katika utukufu”.***

Majira ya urithi

Ni wakati gani Mungu ***“anawaleta wana wengi kwa utukufu”?*** Ni wakati Yesu atakaporudi na tupokee mwisho wa urithi wetu, ***“ukombozi wa mwili wetu”? (Rom 8:23b)*** lahasha! Ukombozi wa mwili ndio utimilifiu wa mwisho wa urithi ulioahidiwa wana. Uwana, kwa njia fupi, inazungumzia kutembea katika ukomavu.

Kutembea kwetu kunaanza tunapo zaliwa mara ya pili (**Yn 1:12-13, 3:3-6)** lakini tunaanza mwendo kama watoto wachanga kufanyika watoto, kisha kuwa mabarehe kwa watu vijana (**1Yn 2:12-14**). Lakini lengo linalotarajiwa ni kufika kiwango cha ukomavu, umri wa kuwekwa kuwa wana. Kuna umri wa kurithi ambao ***“sehemu ya mali inayoniangukia”*** **Lk 15:12,** ***“uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu, ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho”*** **1 Pet 1:4-5,** inapeanwa kwetu; inafunuliwa ndani yetu! Ni ufunuo unaoendelea kufunguka; ni kutembea kwa utimilifu! Kwa utukufu!

Kazi za kwanza za Roho

Sisi ni warithi tangia tunapozaliwa mara ya pili lakini ***“mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote; bali yu chini ya mawakili na watunzaji, hata wakati uliokwisha kuamuriwa na baba”*** **Gal 4:1-2.** Tumekombolewa kutoka kwa sheria na mwana wa Mungu, ili tupokee kufanywa wana **aya 5**. Kwa kuwa tu warithi wa Mungu **aya 7**, hatima yetu ni kuwekwa mahali petu kama wana.

Tunapopokea Roho wa Mungu kwanza tunazaliwa tena na kulingana na ushuhuda wa maandiko, tunaweza kupokea ujazo wa Roho mara moja, kama katika **Mdo 8:14-17** na **Mdo 19:6.** Ujazo wa Roho ni kipawa ambacho Petro aliahidi wale wote waliolipokea neno kwa furaha na wakabatizwa **mdo 2:38, 41**, na karama ile wakristo waliotahiriwa pamoja na Petro walitambua katika **Mdo 10:45**. Lakini sio kuzaliwa mara ya pili [utendakazi ya roho] wala kupokea kama ya roho iliujazwe [utendaji kazi mwingine wa Roho] inatoshana na kufanywa wana.

Kuwekwa pahali pako kama mwana

Kuwekwa kama mwana ni kazi ya ziada [utendaji kazi ya tatu] na kudhihirishwa kwa Roho katika maisha ya mwaamini. Ni kufanywa mwana na roho ambayo inamleta mwaamini katika urithi, katika kutembea katika ukomavu, lengo ikiwa; **kutembea katika utukufu wa Mungu”,** ambao ni **“*Kristo ndani yetu*”** akidhihirika kikamilifu (**Kol 1:27 & Yn 14:21-23).**

Katika uhakika wa kiroho kuja katika uwana sio kuja katika uhusiano wa baba wa kitume lakini ni kumpokea mtume ambaye anahudumu ujumbe na kupokezana uwana. Hata hivyo kama mtu aliyezaliwa mara ya pili anavyo weza kuwahudumia wengine waje katika ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili, na pia kama mtu aliyejazwa na Roho anweza kumleta mwingine katika ujuzi wa kupokea Roho Mtakatifu, ndivyo ilivyo kwamba mwamini ambaye ana ujuzi wa uwana anaweza kuhudumu uwana kwa wengine kwa maana ni utendaji na kupokezwa kwa Roho.

Mitume ni akina baba

Katika miaka ya hivi punde Mungu amerejesha mitume na mitume ni akina baba kwa mwili wa Kristo. Lakini katika urejesho, mitume mara kwa mara ni akina baba haswa kwa huduma ya uongozi na wazee [wazee kulingana na maandiko ni wachungaji viongozi wa makanisa ya pahali pamoja]. Hata hivyo kosa moja ambalo limeenezwa na kutendwa na baadhi ya mitume ni kwamba baba wa kitume anajiweka pahali palipoinuka, akitaka wengine wote waje katika uhusiano wa uwana naye. Mafundisho ya uwana ambayo mitume kama hawa wanapatiana ni kwamba uwana ni jambo linalopatikana kumpata baba wa kitume na kwamba ufunuo wa uwana umefunganishwa na inapatikana tu kwa kuwa na uhusiano wa baba na mwana na mtume huyo.

Hakuna msingi wowote wa mafundisho kama hayo. Ndio, wazi Paulo anamwita Timotheo ***"Mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana"*** **1Kor 4:17,** na Paulo anamwita Tito "***Mwanagu katika imani tuishirikiyo"*** **(Tito 1:4),** na Paulo anasema kwa Onesimo "***mtoto wangu niliyemzaa katika vifungo vyangu",*** **(Filemoni 10).** Vile vile Paulo anafunua kwamba alikuwa baba kwa kanisa la Korintho "***niliyewazaa katika Kristo"*** **(1 Kor 4:15)** na anawaita Wagalatia "***vitoto vyangu"*** **(Gal 4:19).**

Hata hivyo katika nyaraka hizo zote Paulo hatumii lugha ya uhusiano anapofundisha mafundisho ya uwana kwa njia ya kuwekwa. Uwana kwa njia ya kuwekwa ni ya waamini wote, iwe ni wana wa Paulo ama sivyo. Kwa mfano, Paulo aliwaandikia Warumi sio kama baba yao katika imani lakini anafundisha juu ya uwana katika **Rum 8:14-17**. Pia katika **Efeso** Paulo anatuambia kwamba "***Tufanywe wanawe kwa njia ya Kristo Yesu (uwana)*** **Efe 1:5,** lakini hakuna pahali popote katika kitabu ambapo amejitambua kama 'baba', au kwa watakatifu katika Efeso kama watoto wake [Paulo alikuwa baba wa kitume kwa kanisa la Waefeso lakini kwa nyaraka yake hafundishi wazi uwana katika msingi wao kuwa watoto wake wa kitume].

Paulo ako wazi: watakatifu wote wamewekewa hatima kuwa wana – wana wa Mungu, sio wana wa mtume.

Mimi ni baba wa kitume kwa neema ya Mungu na wito wake na karama. Ninao watoto wengi wa kiroho; ninawainua wana katika huduma; nina wana ambao wamekomaa na kuwa akina baba. Katika kikundi cha kitume cha SHILOH tunafurahia ushirikiano huo wa kitume. Lakini funguo ya hayo yote ni **tumepokea roho wa kufanyika wana [Uwana]** kutoka kwa Mungu kwa Roho wake kupitia Yesu Kristo, na sisi wote tu wana wa Mungu ***"kwa njia ya imani katika Yesu Kristo"*** **Gal 3:26**

Tumeitwa kutembea katika ukomavu

Hakuna mmoja wa mitume ambao Mungu ameinua siku hizi za mwisho ambaye amekamilika na hakuna mmoja aliye na ufunuo kamili wa kusudi la Mungu la milele, kwa njia nyingine zaitwa siri au hekima iliyositirika. Hata Paulo alitangaza katika **Wafilipi 3:12**. Wakati huo huo Paulo analiita kanisa litembee katika ukomavu, kupokea "***ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu"*** **1 Kor 2:7.** Ni ***"siri ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote"*** **Efe 3:9.**

Paulo anatuambia katika **Wafilipi 3:15-16** kwamba kuna "nia" ambayo wale wamekomaa wanastahili kuwa nayo; [katika ufahamu wa sasa 'nia' hii ni himaya au mawazo yaliyo kubaliana yakiwa na msingi wake katika ufunuo]. Kama tutakubali kutembea huku katika

ukomavu na kujipatiana kwa "***kueneda katika lilo hilo"*** na ***"na tuwaze hayo"*** kisha Paulo anasema kuwa ***"hata mkiwaza mengine katika jambo lolote, Mungu atawafunulia hilo nalo".*** Hii ni ahadi: Mungu atatutendea; atatuwezesha kutembea pamoja kwa nia iliyo komaa.

Ni kutembea katika neema

Moja wapo wa mtazamo wa ajabu na jambo la muhimu la urithi ni upatianaji wa neema kwetu katika Kristo Yesu. Paulo akisema neema ilipatianwa kwetu kabla ya mwanzo wa nyakati **2 Tim 1:9** na pia anasema katika **Rum 1:5** kwamnba ***"katika yeye tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani, kwa ajili ya jina lake".*** Ni neema ya Mungu tuliopewa bure ndani ya Kristo Yesu ambayo inatuwezesha kutembea katika ukomavu.

Neema hii inahudumiwa kupitia mitume ambao Kristo ameinua katika siku za mwisho kulileta kanisa katika ukomavu, hata utimilifu, ***"hata kufika kwenye cheo cha utimilifu wa Kristo"*** **Efe 4: 13b.** Katika **Efe 1:5-6** Paulo anasema kwamba hatima iliyowekwa ya wana ni "***kwa sifa ya utukufu wa neema yake".*** Ni kwa neema ya Mungu pekee ambapo tunaweza kutembea katika ukomavu. Kufanyika kwetu kuwa wana au kuwekwa mahali petu kama wana ni kazi ya Roho ambayo inatuleta katika neema inayotuwezesha bila kipimo.

Baraka kuu za kiroho

Moja wapo ya ***"Baraka za kiroho"*** ambazo ***"Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ametubariki"*** ni ***"alitangulia kutuchagua ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake"*** **Efe 1:3,5.** Mungu ametuchagua ***"katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu"*** **aya 4** kwa kusudi hili.

Tumewekewa hatima ili tufanywe wana na Yesu Kristo kwake mwenyewe. **Hii ni kiingilio cha, mwanzo wa, kutembea katika ukomavu, na kwa utukufu.** Hii ni kuwekwa na Roho kupokea urithi ulioahidiwa. Sehemu hii katika **Waefeso** imeiweka wazi kwamba Mungu katika Yesu Kristo anatupokea kama wana. Ni kwa kufanywa lakini ufahamu wa kawaida wa neno kuwekwa pahali pako sio maana ya kibiblia ya hilo neno. Neno la kibiblia linamaanisha 'kuwekwa kwa mwana pahali pake'.

Ni Mungu anayetupokea kama wana. Hii inathibitishwa katika **Warumi 8:15** ambayo inasenma "***mlipokea roho ya kufanywa wana".*** Lengo la Mungu ni kwamba baba awe na wana wengi na amewezesha kupitia mwana wake, Yesu Kristo.

Kuingia kwa uwana ni kazi ya neema kupitia Roho

Hatuwezi kufanya kazi ili tuingie kwa uwana hata kama vile hatuwezi kufanya kazi kuupokea wokovu wetu wa kwanza **Efe 2:8**. Kila kitu tunachokipokea kutoka kwa Mungu ni kwa njia ya imani; sio kazi yetu; ni karama ya Mungu. Sio kazi zetu ili mtu ajivune. Ni wakati wa kanisa la Mungu lote kusikia wito wake kuja katika nyumba ya Baba.

Hatimaye kuna nyumba moja tu [kanisa] na ndio nyumba ya Baba. Mungu amewainua mitume siku hizi za mwisho kuliongoza kanisa lake nyumbani. Kazi ya Roho siku hizi za mwisho ni kuwaleta watoto wa Mungu, watumishi wa Mungu, katika uhusianao waajabu na wa uwana kwa Baba. Uhusiano kama huo unawaleta watakatifu binafsi na wahuduma katika uhakika wa ajabu wa usalama, ujasiri, urudi, na kitambulisho kupiia Roho wa uwana au kama Paulo asemavyo katika **Wagalatia,** "***Roho wa Mwanawe"*** **(Gal:4:6).**

Umoja ndilo lengo

Tunapokuja nyumbani na kupata pahali petu katika nyumba ya Baba, kisha tunakuwa mmoja na waamini wengine wote kwa maana tumekuja katika ukomavu; tumepokea "***umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu";*** tumekua mpaka ***"mtu mkamilifu hata kufika kwenye cheo cha utimilifu wa Kristo"*** **Efe 4:13.** Kuja huku katika umoja itawezekana tu wakati mitume ambao wameitwa na Kristo kulea na kuongoza kanisa wamekuwa na nia **moja,** wakifuata **shauli moja** na **kuwa mfano** kwa watakatifu wafuate, **Wafilipi 3:16-17.**

Watu mfano

Paulo anaongea juu ya kikundi kikieneda katika ukomavu katika **Wafilipi 3:15-17**. Katika **aya15** Paulo anasema ***"basi sisi tulio wakamilifu na tuwaze hayo";*** kuna makubaliano ya kuingia ndani yake kama wafuasi wa Kristo waliokomaa. Kisha Paulo anasema ***"na hata mkiwaza mwngine katika jambo lolote, Mungu atawafunulia hilo nalo";*** mara tunapokubali na kuingia katika ukomavu, kutakuwa na baadhi ya mambo ambayo hatujui na hatukubaliani, lakini Paulo anatuhakikishia kwamba Mungu atatupatia ufunuo ili ***"tuenede katika lilo hilo"*** **aya 16.**

Kisha Paulo anasema ***"mnifuate mimi"*** na ***"mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi"*** **aya 17.** Katika siku hizi Mungu anainua 'watu mfano', ambao wataonyesha njia ya Bwana, ndani na kupitia ambao Bwana atajithihirisha kupitia kwao, na ambao kupitia kwao utendaji kazi wa mwili wa Kristo utaonekana.

KUJUA NEEMA YA MUNGU

Martin Luther – kufanywa upya

Wakati Martin Luther (mapema kalne ya 16) **alitambua neema ya Mungu ya kuokoa kupitia imani katika neno la Mungu,** alifanyika mpinzani, sio tena kuendelea na tabia na kazi za kanisa Katoleki ya siku zake. Kazi ya urejesho na uhuisho ilikuwa imeanza na ilikuwa ni urejesho wa elimu ya Mungu (Theologia).

John Wesley – kuzaliwa upya

Wakati John Wesley [kalne ya 18] **alihisi 'uamsho usio wa kawaida' kwa mahubiri yalioongozwa na Roho** ya ndugu wa Moravian katika Aldersgate- Court, hakutegemea tena 'njia' yake ya utakatifu ambayo alikuwa amebuni akiwa chuo kikuu, lakini sasa **akahubiri kwa uhuru neema ya Mungu na akaona maelfu maelfu wakipokea kuzaliwa upya.** Huu ulikuwa ni urejesho na kufanywa upywa kwa kupatana kwa undani na Mungu.

Reverend Seymour – uhuisho wa kipentekote

Wakati Rev Seymour na wengine walikusanyika katika barabara ya Asuza, Los-Angeles, **mwaka wa 1906, kungojea Bwana kwa kujazwa na Roho Mtakatifu,** walibarikiwa kwa nguvu na kufanywa upya kwa Roho, kwa ishara za nguvu, haswa ndimi. Toka hapo **uhuisho wa kipentekote imeguza mamilioni ulimwenguni** na kwa mda mrefu imekuwa ndio sehemu ya kanisa ambayo imekua kwa kasi.

Mwondoko wa kiroho/ charismatic

Kutoka mapema 1960 kwenda mpaka mapema 1980 Mungu aliachilia mwondoko mwingine wa nguvu za Roho na **Mamilioni walijazwa na Roho Mtakatifu kupitia kuwekewa mikono.** Hile inayoitwa mwodoko wa kiroho iliwasongesha waamini katika safari ya urejesho na kufanywa upya.

Roho wa kufanywa wana.

Katika siku zetu Bwana anamwaga Roho wake tena lakini kwa njia tofauti na ya kipekee: anamwaga **Roho wa kufanywa wana** ambapo tunafanyika wana wa Mungu kupitia Yesu Kristo (**Efe 1:5**). Hii ni ***"kwa sifa ya utukufu wa neema yake"*** **Efe 1:6.** Huu ni ujuzu wa kuja kwa maeneo na uhakika wa neema ya Mungu, ambayo kwanza haikujulikana na wateule hata haikujulikana na wahuduma wa kiroho ambao wanathihirisha vipawa vya nguvu lakini wasijue uhusiano wa undani na mabadiliko ya ndani ambayo yameletwa na ujuzi wa neema ya Mungu kwa kufanywa wana. Hii inatiwa ndani yetu na Roho, ikiachilia neema (nguvu za kutuwezesha) kutembea katika uhusiano wenye ukomavu na Mungu kama Baba na sasa tukiweza kupokea urithi ambao umewekwa mbingini ***"ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho"*** **1 Pet 1:4-5.**

Huiothesia = kufanywa wana

'Neno kufanywa wana' linapatikana mara tano katika agano jipya katika maandiko ya Paulo: **Rum 8:15, 23; 9:4; Gal 4:5; Efe 1:5.**

'huiothesia' SC#5206, *Inamaanisha 'kuwekwa kwa mwana mahali anopostahili, hivyo ni kufanywa wana ; uwana katika heshima ya Mungu'.*

Vines Expository Dictionary yasema:

- Neno hili *'linaonyesha pahali na hali ya mwana akipeanwa kwa mtu ambaye haikumpasa;*
- *Roho Mtakatifu anatengeneza ndani yao* (watoto wa Mungu) *ufahamu wa uwana na nia ya wana.'*
- *'Uwana unawekwa kutokana na uhusiano ambao unakuja kwa kuzaliwa'* Gal 4:1
- Kuna utofauti kati ya *'Uwana wa mwaamini na uwana uliotangulia wa Krsto'.*
- *'Mungu hawapati waamini kama watoto; wanapatianwa na Roho Mtakatifu kwa njia ya imani'.*
- '*kufanywa wana ni msemo unaohusisha heshima ya uhusiano wa waumini kama wana;*
- *Sio kwa kuwekwa kwa jamii kwa kuzaliwa kiroho, lakini kuwekwa pahali unapostahili kama mwana'.*

[Vines Expository Dictonary, Unabridged edition, riverside book na Bible housu Page 34].

Nimeshiriki mawazo haya ya vines kwa maana yanaleta uwazi katika ufahamu. Kila mtoto wa Mungu aliyezaliwa tena ni mrithi na ndio, wengi wangesema tayari 'mwana'. Hata hivyo uwana ni jambo ambalo tunakuwa ndani yake na hivyo wakati unakuja wa kupokea roho wa kufanywa wana, sasa tukitembea katika ukamilifu.

Ujuzi wa tatu

Tunazungumzia juu ya '**ujuzi wa tatu'** ambao ni utimizo wa sikukuu ya tatu, sikukuu ya mabanda. Jambo kubwa la kufahamu katika sikukuuu ya mabada ni 'makao' inamaanisha 'pahali pa kudumu'. Kutimizwa kwa sikukuu kunalenga watakatifu wakifanyika '**makao [mahali pa kudumu]'** pa Mungu. Hii inaongea juu ya watakatifu wakitembea katika ufunuo wa siri ***"nao ni Kristo ndani yenu*** **[Kristo akidumu/ akifanya makao ndani yenu]** ***tumaini la utukufu"*** **Kol 1:27**

Mungu alifanya mabada katika hali ya mwanadamu

Yohana 1:14 inasema **"*Naye neno alifanyika mwili, akakaa [akafanya makao] kwetu; nasi tukauona utukufu wake; utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli".*** Yesu alijivika mwili mnyonge wa mwanadamu lakini ajapofanya hayo, **utukufu wa Baba ulifunuliwa katika hali ya mwanadamu na ikaonekana duniani.** Huu ulikuwa ndio mwanzo wa kutimizwa kwa kusudi la Mungu

Yesu ametuandaa tuwe makao

Katika **Yohana 14:2** Yesu alisema ***"Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi*** [mahali pa kudumu, makao***]; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali [***mahali pa kudumu]". Wakati wengi wadhani kuwa Yesu anazungumza juu ya mahali pa kudumu siku za baadaye mbinguni, ukweli ni kwamba Yesu alikuwa akienda msalabani kushughulikia dhambi mara moja na ya kutosha na kupitia kupatia kwa ajabu damu aliomwaga, aliwatakasa waamini kutoka dhambi yote, akiwafanya wawe mahali pazuri pa Mungu pa kudumu ndani ya Roho.

Baba na Mwana watadumu ndani yetu

Yesu anaendelea katika **Yohana 14:23** anapoahaidi ***"Mtu akinipenda atalishika neno langu [lagos, neno lililoandikwa]; na Baba yangu atampenda, nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake".***

Neno lililotumika la 'makao' {SC# 3438 *mone* inamaanisha pahali pa kukaa, makao [kitendo cha kudumu au makao] imetafsiriwa makao katika **Yohana 14:2** na neno lile limetumika katika **aya 23** na kutafsiriwa 'nyumba' au 'kikao'}. Haizungumzi juu ya makao ya mbinguni lakini kwa makusudi ya Mungu kumjaza mwaamini kikamilifu, ukae naye au adumu ndani ya mwaamini. Lengo la Mungu limerejerewa wazi katika sehemu nyingi katika agano jipya na imeelezwa wazi katika agano la kale: **lengo lake ni kufunua utukufu wake ulimwenguni kupitia watu wake.**

Sikukuu za waisraeli zinatufundisha kusudi la Mungu linaloendelea kufunuka

Hata kipindi cha kanisa kilipoanza kupitia Yesu akitimiza pasaka na akitupa wokovu wetu, na akimtuma Roho mtakatifu katika kutimiza pentekote, hivyo akitupa nguvu kwa kushuhudia, ili sasa katika mwisho wa kizazi cha kanisa Yesu Kristo analileta kanisa lake katika kutimizwa kwa sikukuu ya mabanda. Kupitia pasaka tunaokolewa kwa imani katika neno la Mungu na kupitia pentekote tunatiwa nguvu kwa sababu ya huduma. Ujuzi huu wote unatuleta katika uhusiano na Mungu unaokua na neno lake, na ujuzi wa pili unajenga juu ya ule wa kwanza.

Kwa hivyo sasa Mungu anawaleta watoto wake, watumishi wake, katika **ujuzi wa tatu** ambao ni ujuzi mkuu wa Mungu akidumu ndani yetu, kujua uhusiano wa ndani na ulio kamilika na Baba na Mwana wake, Yesu Kristo – kutimizwa kwa **Yohana 14:23**, na uhakika wa ushirika wa kitume ambao hakika ni ***"ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo"*** **1 Yn 1:3.**

BARAKA TANO ZA BABA

Miaka kadhaa iliopita, baba wa kitume akifundisha SHILOH [kituo chetu cha mafundisho katika Toowoomba, Australia] alitaja alipopitisha Baraka tano ambazo baba anaweza kuwapa wana/ watoto wake. Bwana alitunenea kwa nguvu kupitia haya na tumeyafanya yetu. Kutoka wakati huo tumeomba kwa kusudi na kupokezana baraka hizi tano mahali kwingi, wakati wowote ambapo tumehudumu neema ya uwana, kwa matokeo yenye nguvu. Baraka hizi tano ndizo ambazo baba wa asiri anaweza kumpa mwanawe /watoto kwa kiwango fulani na ni ukamilifu wa baraka hizo ambazo Mungu Baba anataka kuwapa wanawe. Hii inaonekana katika kiroho kama wandugu wanapoingia katika neema ya uwana.

Baraka hizi tano ni: ushujaa, usalama, nidhamu, kitambulisho, kufaulu.

Ushujaa

Huu ni **ujasiri wa kusimama ndani ya Kristo** katika kila mahali na kulitangaza jina lake, ukiwa mwaminifu kwa neno lake. Mfano wa baba akipatiana ushujaa kwa mtoto wake ni kama ifuatavyo: kijana mdogo amedhulumiwa kwa uwaja wa kucheza. Hata hivyo baba yake anakuja shuleni, na yule kijana mdogo akiwa ameshikwa mkono na baba yake, anawashambulia walio mdhulumu akiwa na ushujaa tosha. Kwa nini? Kwa kuwa baba yake amesimama pamoja naye; haogopi tena na ana ushujaa wa kukabiliana nao.

Wakati Bwana alinitokea 01/1998 kabla tu hatujaanza huduma ambayo tunafanya kazi nayo leo, aliweka ndani yangu **'ushujaa'.** Nilihisi uoga kwa kuwa tulikuwa tunatoka kwa dini/ kanisa ya idara ya mipangilio kwa mara ya kwanza na nilikuwa niwe kiongozi. Nilipokea ushujaa unaoweza kuguzwa kutoka kwa Yesu. Alidhibitisha haya katika **Yoshua 1:1-9** ambapo ushujaa na uhodari zinatajwa mara tatu. Neno kuu lilikuwa katika **aya 6** ***"uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa nchi hii niliowaapia baba zao ya kwamba nitawapa".*** Toka wakati huo, kama yule kijana uwajani, nimekuwa nimejaa ushujaa kupitia Roho wa Mungu kwa kuwa ninajua Baba yangu anasimama pamoja nami.

Usalama

Hii ni **kujua kwamba 'mimi ni wa'.** Watu kokote wanatafuta usalama na kiutamaduni wamepata usalama katika jamii, katika tamaduni, katika kampuni wanazofanyia kazi na mengine kama hayo lakini usalama huo haupatiani usalama unaofaa kwa mtu binafsi. Wachungaji na viongozi wengi ambao wamekuwa katika huduma kwa miaka mingi hawajakuwa na usalama. Hii inaonekana kwa njia ambayo wanafanya kazi na hii ni kwa njia ya kutawala. Katika ujuzi wangu nilikuwa kimawazo sina usalama mpaka nilipotimiza miaka 51. Wakati nilipokea Roho wa kufanywa mwana ambapo nilikuja katika uhakika wa uwana kwa Mungu, nilivyo jihisi mara hio ilikuwa 'nina usalama kwa mara ya kwanza katika maisha yangu'; nilielezea haya kama 'nimekuja nyumbani'. Nilikuja nyumbani kwa nyumba Baba.

Jambo kuu katika usalama ni kukubalika na Mungu anawatumia akina baba wa kitume kuonyesha kukubalika huko kwa watoto wake. Hakuna tena jambo hilo la kung'ang'ana na kushindana na wengine au kujidhibitisha. Usalama hutoka ndani na unaleta uhuru wa yule ambaye unastahili kuwa. Sisi ni wa nyumba ya Mungu, nyumba ya Baba yetu, na kama wana

tunatambua sisi tunasehemu: sisi ni wana kwa Baba. ***"Akaondoka akaenda kwa babaye alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana"*** **Lk 15:20.**

Nidhamu

Katika jamii za wakristo tunatarajia baba kuchukua wajibu wa kimsingi wakuleta nidhamu. Wakati haya yametendeka vyema watoto wanakua katika hali nzuri ya nidhamu na watapokea nidhamu hiyo kama yao watakapokomaa. **Ebr 12:3-11** inazungumzia urudi wa wana. Mungu kama Baba Yetu ni mpole kwa watoto wake lakini anakuwa mkali na wana wake, ambao wamekomaa.

Matokeo ya urudi wa Baba itatuleta pahali ambapo tuko miongoni mwa ***"wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu"*** **Rum 8:14. Uhakika wa urudi wa kiungu ni kuishi na kutembea ndani ya Roho** kwa hivyo maandiko yanasema ***"basi si afadhali sana kujitia chini ya Baba wa roho zetu na kuishi"*** **Ebr 12:9b.** Mara tu tunapotembea katika uwana, tunaweza kuisikia sauti ya baba tayari sana na kuwa tukifanana na Yesu, tukifanya tu "***Lile ambalo amwona Baba analitenda"*** **Jn 5:19.**

Baba anatamani watoto wake wapewe nidhamu katika maisha yao. Baba yetu anatamani tuwe na nidhamu katika kulisoma neno lake, katika kutumia muda naye katika maombi, katika bidii za kukua katika karama, lakini zaidi Baba anataka tutembee katika urithi ***"uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu, tayari kufunuliwa wakati wa mwisho"*** **1 Peter 1:4-5.** Tunapopokea Roho wa kufanyika wana Baraka hii ya urudi inakuja maishani mwetu na inatuwezesha kwenda katika utimilifu katika kutembea katika ukomavu.

Kitambulisho

Hii ni, **kujua 'wewe ni nani'.** Watu hujificha katika vitambulisho nyingi, wakati mwingine katika nywele za kubandikwa au katika miundo mipya ya mavazi. **Kitambulisho chetu ni katika uhakika 'hatima yetu ikifunguka'.** Biblia inaiweka wazi kwamba Mungu ametuwekea hatima ***"Ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo"*** **Efe1:5;** ***"tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza tuenede nayo"*** **Efe 2:10;** na ya kwamba kuna ***"Mashindano yaliowekwa mbele yetu"*** **Ebr 12:1.** Mashindano haya yanajulikana vyema kama 'njia ya maisha yetu ambayo tayari Bwana ametupangia'.

Hata kama vile mke alichukuavyo jina la mumewe na anapata kitabulisho kama mke, na hata watoto wanavyoitwa kwa jina la baba yao, hivyo akiwatambua, hivyo ndivyo iliyo kwa watoto wa Mungu. Tunapata kitambulisho chetu kutoka kwa baba yetu, lakini uhakika wa kitambulisho kamili inajulikana tu kwetu wakati tunakuja kwa uwana.

Sehemu kuu ya uwana ni ile hali ya 'kumiliki'. Sisi sio watumwa katika nyumba lakini wana kwa njia ya urithi. Mabadiliko haya yanabadilisha nia zetu katika huduma, sio tena kutumika nyumbani kama watumishi lakini kumiliki na kuwajibika kama mwana.

Kuna nguvu kuu na mamlaka zinazoachiliwa unapojitambua na kuweza kusimama na kutangaza 'mimi ni mtume waYesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu'! [Ama kila huduma iwayo yote, ambayo Mungu ameiweka ndani yako].

Kufaulu

Haya ndiyo matunda ya mwisho ya baraka za Baba. **Wakati baba anambariki mwana, yeye anatia ndani yake kukubalika na neema kwa mwana kufaulu.** Moyo wa baba wa kweli ni kuona kwamba wana wamefaulu hata zaidi ya baba.

Wengi wetu hatujapata Baraka za baba zetu wa asiri kuondoka katika maisha na kufaulu na jambo la kuhuzunisha wengi wetu katika huduma za kanisa hawajabarikiwa na baba wa kitume. [Yakobo aliwabariki wana ya Yusufu, **Mwanzo 48:1-20**. Huyu alikuwa baba wa kiasiri na wa kiroho akiwabariki wana.]

Bwana asifiwe, anawainua baba wa kiroho leo na kuwawezesha kuachilia baraka kwa wana katika huduma. Akina baba kama hao wanaridhika kikamilifu wakati wana wao wanaweza kufanya kazi kwa uhuru kutoka kwa baba, wakifanya kazi ambayo baba angelipenda ifanywe lakini hawezi kuifanya. Haya yameanza kutendeka sasa.

Umekuwa ni ujuzi wetu kwamba wengi, ambao wana wito wa kiroho katika mioyo yao, wanahitaji ‘baraka’ za kuambiwa ‘unaweza kutenda’; utafaulu katika katika yale Bwana amekupatia kuyafanya’. Baraka za Baba sio tu kwa wana katika huduma lakini ni baraka ambazo kila mtoto wa Mungu anahitaji wakati wamekomaa na wamefika umri wa uthi.

Ombi:

Baba uliye mbinguni, ninakuomba uniongoze kwa neema na Roho wako Mtakatifu kufahamu na kuingia katika uwana.

Ninatambua kwamba ni wakati wangu wakukomaa, kutambua kwamba nimekomaa kupokea urithi kutoka kwa Baba yangu kupitia Kristo Yesu.

Bwana ninakushukuru kwamba uliniita kuwa mwanafunzi wako na nimejifunza neno lako kwa bidii.

Bwana ninakushukuru kwamba umeniita kuwa mhuduma wako na nimetafuta kukutumikia kwa kila njia.

Ninatambua kuwa sasa ni wakati wangu kuwa mwana. Ninaomba neema ya kuelewa; ninaomba ufunuo wa kujua; ninaomba upako wako wa kugeuzwa.

Bwana ninataka kuwa mwana wako. Ninataka kupokea ushujaa ndani ya moyo wangu ili niweze kusimama kwa ujasiri kwako.

Ninatamani kuwa na usalama kama mwana wako na sasa, kama mwana wako; nisinga'ng'ane tena au kujithibitisha; ili niwe na usalama ndani yako na katika mwili wako.

Najiachilia kwa marekebisho ya Bwana kama mwana. Nikijua ya kwamba kama Baba yangu, utanileta kwa ukamilifu kupitia kwa nidhamu yako ya kiungu.

Bwana, nifunulie kitambulisho changu ninapotembea katika uwana, nikipokea urithi wangu na kutimiza wito wa Mungu katika maisha yangu.

Bwana ninaomba Baraka zako juu ya maisha yangu kuniwezesha kufaulu katika maisha.

Baba, 'nipe kile ambacho umekuwa umeniwekea', kabla ya nyakati kuanza.

*AMINA***.**

UOMBEZI MKUU

Viumbe vyote na watakatifu waliozaliwa na Roho

"Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa. Wala si hivyo tu; ila na sisi wenyewe tulio na malibuko ya Roho, sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukikutazamia kufanywa wana, yaani ukombozi wa mwili wetu" **Rum 8:22-23.** Hii inaongea juu ya maombezi makuu ambayo viumbe vyote na watakatifu waliozaliwa na Roho wanahusika ndani yake. Ni kuugua na utungu wa kuzaa; jambo ni lazima lizaliwe; maisha mapya ni lazima yapatikane, ambayo haitaguza tu viumbe na kuikomboa kutoka kwa laana lakini itawaachilia watakatifu katika utimilifu wa uwana – **ukombozi wa mwili.**

Yesu ndiye mwombezi mkuu

Yesu, mwana wa Mungu, ndiye mwombezi mkuu na ***"zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea"*** **aya 34.** Wakati Yesu alikufa msalabani ***"mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa, ambayo kwa hayo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri"*** **1Peter 3:18-19.** Yesu sasa ndiye kuhani mkuu "***aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai siku zote ili awaombee"*** **Erb 7:25.**

Yesu alifanya maombezi katika kilindi cha dunia

Petro alipohubiri katika siku ya pentekote alipatiana hadithi ya ajabu kumhusu Yesu mtu katika **Mdo 2:22-24**:

- **Aya 22**, Anaongea juu ya huduma isio ya kawaida ya Yesu, ***"mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara"***
- **Aya 23,** anazungumzia kifo chake kama kusulibishwa.
- **Aya 24,** anaongea juu ya kufufuka kwake.

Tafsiri mpya ya biblia ya mfalme yakobo inasema Mungu alimfufua Yesu, ***"akiufungua uchungu wa mauti";*** NAS Bible ***"Uchungu wa mauti".*** Hata hivyo neno la Kiyunani linamaanisha '*utungu wa kuzaa'.*

Utungu wa kuzaa

Wakati Yesu Mwana wa Mungu alikuwa katika kaburi kwa siku tatu mchana na usiku, hakuwa katika mapumziko, pia hakuwa akiteswa na mapepo ya kuzimu. Alikuwa ndani ya roho na alikuwa akitimiza kazi ya ajabu ambayo ni Mungu tu (Katika mwili) angalifanya. Petro anasema alikuwa akipitia **utungu wa kuzaa,** hivyo ni, **uombezi mkuu,** kuleta uzima toka mauti, kwa ***"maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa"*** (**1 Kor 15:53**).

Mazao ya maombezi yake

1. Yesu ndiye libuko la wale watakaofufuka katika wafu (**1Kor 15:20**).
2. Yesu alikuwa akizaa viumbe vyoye vipya!
3. Yesu alikuwa akiyashinda mauti katika mwili – akiondoa hukumu ya dhambi za mwanadamu.
4. Kupitia kufufuka kwa Yesu tunapokea uzima wa milele tunapozaliwa mara ya pili.

Uhuru wenye utukufu haujafunuliwa

Kulingana na **Rum 8:20-21,** ***"viumbe vyote pia vilitiishwa chini ya ubatili, ila…katika tumaini".*** Viumbe vyenyewe ***"vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu". 'Uhuru huu wa utukufu'*** *ni nini?* viumbe vyawezaje kukombolewa kwa kitu ambacho hawajakipitia wana wa Mungu? **Aya 19** imetuambia yakwamba ***"viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu".***

Hapo mbele maandiko yametuambia kupitia Kristo tumepokea roho wa kufanywa wana (uwana) **Rum 8:15** na kuwa ***"sisi tu watoto wa Mungu"*** **aya 16.** Kama tu watoto wa Mungu, basi tu ***"warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo"*** **aya 17.** Hata hivyo ***"mrithi, wakati wote awapo mtoto hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote; bali yu chini ya mawakili na watunzaji, hata wakati uliokwisha kuamuriwa na baba"*** **Gal 4:1-2**

Paulo mtume aliyafahamu maombezi haya makuu

Uombezi huu mkuu ni nini? Yesu amekwisha kufufuka katika wafu na uhakika huo na ukweli ni usalama wa imani yetu. Ni kupitia maombezi yake katika Roho – '***utungu wa mauti'*** viumbe vipya vilifanyika hakika. Ni nini zaidi, Yesu ***"yu hai siku zoye ili awaombee ambao wanaokolewa"*** **Ebr 7:25.**

Lakini kitu zaidi ni lazima kitendeke, hivyo ni, *"****kufunuliwa kwa wana wa Mungu"*** **Rum 8:19.** Paulo anasema kwa Wagalatia ***"vitoto vyangu ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu"*** **Gal 4:19.** Paulo anazungumzia wakristo walio watoto katika ufahamu wao. Paulo inamuiga Kristo na uombezi huu mkuu akiugua katika utungu wa kuzaa mpaka '***kristo aumbike'*** **-** wana wanathihirishwa! Watoto wamekua mpaka kwa ukomavu!

Kuwaleta wana wengi kuufikia utukufu

Uombezi mkuu ni nini? Ni kuumba kwa ***"Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu"*** **Kol 1:27.** Hayo yanapotendeka kupitia kumhubiri Kristo ***"tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo"*** **aya 28,** mahubiri yatafanya kazi kwa sababu ya maombezi makuu ambayo watakatifu na haswa wahuduma wanaingia kwake kuona kufanywa wana kikamilifu imetendeka.

Lengo ni ***"kuleta wana wengi waufikilie utukufu"*** na haya yanawezekana kwa sababu Yesu Kristo tayari amefanyika ***"kiongozi mkuu wa wokovu wetu",*** akiisha ***"kukamilishwa kwa njia ya mateso"*** **Ebr 2:10.** [Tayari nimeshiriki maana ya ndani ya utungu wa kuzaa **Mdo 2:24**].

Hata kama Yesu alivyokamilishwa kwa mateso aliyoyapitia vivyo hivyo ni lazima tukumbatie na tustahimili mateso ambayo hakika ni mlango na njia ya utimilifu. Urithi ni utukufu! Lakini kama warithi pamoja na Kristo ni lazima pia "***tuteswe pamoja naye"*** **Rum 8:17.**

Viumbe vyote ***"vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa.*** Viube vililaaniwa kwa sababu ya anguko la mwanadamu lakini, "***katika tumaini".*** Hatuifahamu lakini kuna uombezi unaoendelea miongoni mwetu katika viumbe na viumbe vinalia kwa ukombozi. Uombezi huu unastahili kushirikianwa na watoto wa Mungu, ***"walio na malibuko ya roho".*** Lengo ni wana wengi watembee katika utukufu wa Mungu. Mungu amekusudia tangia mwanzo dunia ijawe na utukufu wake.

Mafundisho ya ziada:

Maandiko yafuatayo yanapatiana mktasari wa kusudi la Mungu la milele katika kuumbwa kwa mwanadamu: **mwanzo1:26-28, Hesabu 14:21, Isaya 40:5, Habakuki 2:14, Kol 1:27, Efe 1:27.** *Tafathali soma maandiko haya. Kuna maandiko mengine mengi: yatafute na uyatafakali*

Ni wakati wa urithi

Ni wakati wa utukufu! Kwa miaka 100 iliyopita kanisa limekuwa likijua nguvu za Mungu. Kabla ya hayo hata wakati wa Luther na kupitia uamsho mkuu wa Wesleyan, kanisa lilikuja kujua uwepo wa wokovu wa Bwana. Lakini sasa ni wakati wa utukufu wa Bwana kufunuliwa ulimwenguni, na **ni wana watakaoletwa katika utukufu.**

Lengo la Mungu kwa watu wake ambao ni warithi kwa kuzaliwa mara ya pili ni juu yao waje katika ukomavu, ***"wakati ulioamriwa na Baba".*** Wakati huo ni sasa! Ni wakati wa Baba kwa kanisa lake kupokea urithi ulioahidiwa ***"usio haribika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho"*** **1Peter 1:4-5.**

Mwili wote unatakiwa uje katika ukomavu

Uombezi mkuu ni wito huu juu ya wale ambao tayari wameelewa siri ile, siri iliofichwa ya Mungu ambayo ni ya wale waliokomaa ***"ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu"*** (**1Kor 2:6-7**) kuingia katika kuugua na utungu ambayo inazalisha ukomavu kwa mwili wa watakatifu. Wakati ambapo uwana unaingiwa na mtu binafsi ni wito wa pamoja kwa kanisa sasa.

Huduma tano za **Waefeso 4:11** zinafanya kazi ya huduma, ambayo ni kuwakamilisha watakatifu [kuwekwa vyema ili kufanya kazi katika mwili] na kujenga mwili wa Kristo mpaka sote ***"tutakapofikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu [***kwa pamoja, mwili wote***] hata kufikia cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"*** **Efe 4:12-13.** Matokeo yatakuwa ni mwili mkamilifu hapa duniani ukifanya kazi kwa nguvu katika upendo wa *agape,* ukidhihirisha kwa wote kuwa Yesu ndiye Kristo [Masihi] Mwana wa Mungu aliye hai.

Tunahitaji kuwa tumetiwa muhuri na Roho Mtakatifu

Ni utukufu wa Mungu ambao unajulikana kwa njia ya ufunuo wa siri ambao unawezesha watakatifu kutembea katika ukomavu [wakiwa na ujuzi wa kufanywa wana, hivyo ni kuwekwa pahali pako na na Roho Mtakatifu katika uhusianao ulio hakika na uhusiano na Mungu Baba, kutembea katika urithi] kudhihirisha asiri na serekali ya ufalme wa Mungu duniani. Roho wa uwana [kuwekwa mahali pako] tayari amewekwa ndani ya mioyo yetu lakini wengi tayari bado hawajaamini utimilifu huu. Twahitaji kupokea ***muhuri*** kupitia Roho kupokea na kutembea katika urithi ulioahidiwa (**Efe 1:14, 2 Kor 1:22**).

Kwa ukombozi wa mwili

Sisi watakatifu tunangojea kwa subira kufanywa wana *"**ukombozi wa mwili wetu"*** **Rum 8:23.** [ukombozi SC# 629 *apolutrosis* inayomaanisha kuachilia, kukomboa, kitendo cha kulipia gharama kamili. Hili neno linatoka kwa neno '*kuwachilia/kufungua'.* Yesu amelipa gharama kamili kupitia damu yake ili tupate kupokea kikamilifu, ukombozi wa mwili.]

Ukombozi wa mwili ni nini ambao tunangojea kwa subira? Katika mazingira ya kifungu hiki ukombozi wa mwili ni sehemu ya kufanywa wana / kuwekwa mahali pako. Kwa hivyo inazungumzia ukombozi kamili ambao ***"awatakase kabisa, nanyi, nafsi zenu, na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama"*** **(1The 5:23).**

Kwa kupokea Roho wa kufanywa wana

Roho wa kufanywa wana ni kuwezeshwa kwa neema kutembea katika uhusiano wa ukomavu na Mungu ukiwa na msigi katika kupokea hekima ya ndani **1Kor 2:7**. Tunapotembea katika uwana ***"Roho wa hekima na ufunuo"*** **(Efe.1:17),** inatuelekeza katika ufunuo unaoendelea kufunguka wa siri**. Efe 3:9** inasema kuna "***ushirika wa siri"***; katika **Kol 1:25-27**, Paulo anasema ufunuo wa siri ni kutimiza neno la Mungu katika watakatifu ambayo hatimaye ***"Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu".***

Gharama yote imelipwa

Tunapojipatiana kwa uombezi huu mkubwa tutakuwa tukiuita mwili wote wa Kristo katika ufunuo wa ***'gharama yote'*** kwa kuwa ukombozi wetu umelipwa na Kristo kupitia sadaka yake ya ukombozi. Ufahamu kamili wa ukombozi sadaka ya ukombozi umeunganishwa na ufahamu ambao kanisa linahitaji kuja katika uhakika kamili wa siku ya upatanisho.

Sasa kupitia kufufuka kwake tunaungana naye katika uombezi mkuu ili kwamba ukombozi ujulikane katika mwili. Mwili unazungumzia hema ya ulimwengu ambayo Paulo anasema inatakiwa kuvalishwa zaidi (**2Kor.5:4**). Huu ni ufunuo wa ndani ambao Mungu anaanza kufunua. Ufunuo huu utapatikana zaidi tunapoingia ndani ya uombezi na Kristo.

Krsito ndani yetu, mwombezi

Maandiko yanaahidi kwamba Roho mwenyewe atatusaidia ***"kutuombea kwa kuugua kusiko weza kutamukwa"*** **Rum 8:26,** ***na "Yeye aichunguzae mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu"*** **Aya 27.** Kumbuka kwamba **Rum 8:34** inamtabulisha Kristo akiwa katika mkono wa kuume wa Mungu akituombea – Mungu ni mmoja: Kristo ndani yetu (Roho) na Kristo akiwa ameketi katika mkono wa kuume! Maombezi haya makuu yaweza kukoma jinsi gani! Ni jambo la Mungu!

Viumbe vinangonjea

Ni wakati wa kuingia kwenye maombezi haya makubwa, kuelewa lengo, kupokea urithi, tukijifundisha kukumbatia na kuomba na kuruhusu Roho kuomba kupitia sisi kuleta wana wengi katika utukufu. Hii ni ***'kufunuliwa kwa wana wa Mungu"*** ambayo viumbe vyote vinangojea kwa kuwa ni kupitia wana waliofunuliwa ambapo viumbe vitakombolewa.

Mungu amekwisha kutupa kionjo cha uhakika huu katika maeneo tofauti ulimwenguni. Kwa mfano, katika kilindi cha Fiji (katika bahari ya WESTERN PACIFIC) miaka michache iliopita kijiji ambacho kijito chake kiliwekwa sumu walitubu juu ya dhami ya wazee wao. Katika karne ya 19 mmishonari mwingeleza kutoka Australia waliuwawa katika kijiji hiki na wazee wao. Kijiji kilimgeukia Kristo katika miaka ya hivi punde na wakawasiliana na uzao wa waingereza wakiwaomba waje kijijini kutoka Australia kwa sherehe ya mapatano ambapo wanakijiji wakiongozwa na wazee/viongozi na wahuduma wakristo wakaomba msamaha kwa dhambi zilizotendwa mwanzo. Msamaha ulitolewa; mapatano yalifikiwa na kwa njia ya miujiza katika siku hiyo kijito kikapata ladha tena. Hallelujah! Kunazo hadithi zingine kama hizi.

Kanisa lililokomaa ndio jambo kuu

Matarajio yetu ni kwamba Mungu ambaye aliumba ulimwengu uwe na mazao na mazingira yenye ukalimu kwa mwanadamu na viumbe vyote alivyoviumba, kupitia wana wake waliofunuliwa ambao wanatembea katika ufunuo wa utukufu wake, waanze kukomboa viumbe na kuachilia viumbe katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu.

Matarajio yetu ni, **kanisa linapoanza kutembea katika ukomavu kwa kutambua kikamilifu na kupokea roho wa kufanywa wana, kanisa litaanza kuwa kanisa lenye utukufu ambalo Kristo anaandaa kujiletea.**

Niwakati wa uombezi mkuu.
Amen!